

MSIOGOPE



Bwana akubariki, Ndugu. Asante sana.

² Asanteni, ndugu, kwa... [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Asanteni. Asanteni. Asanteni. Ninataka kusema, “Asanteni, ndugu zangu wapendwa,” kwa ajili ya utangulizi huu. Nisingeweza kuwa na uhuru zaidi na kujisikia siko nyumbani zaidi ya kama ningekuwa kwenye mimbara yangu nyumbani. Mungu awabariki. Nipo hapa kwa kusudi la kuweka juya yangu pamoja na zenu kusaidia kwa yote tuwezayo kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, kumshika kila mtu anayepotoka na kumwacha Mungu. Hakika ninawashukuru kwa ajili ya jambo hilo, na ninatumaini ya kwamba mtakuwa mkiniombea ninapohudumu. Wala hakuna kitu kilicho bora zaidi kuliko msingi mzuri unapowahudumia watu wote katika...?... Bwana awabariki.

³ Habari za jioni, marafiki. Nina furaha sana kuwa hapa tena, usiku wa leo, katika jumba hili kubwa la mikutano la mahali hapa pa mifugo, ama, pa maonyesho. Nafikiri hii ni yapata mara yangu ya tatu kuwa hapa, na kila wakati sikuzote imethibitika kuwa ni baraka nyingi kuwa hapa, na kukutana na watu hapa wa California.

⁴ Ninawaletea, usiku wa leo, heri nyingi na baraka kutoka kwa ndugu wa mashariki, na kanisa lililoko mashariki, kuwaambia ya kwamba wanaendelea vizuri chini ya majaliwa makuu ya Mungu, na kutumaini ya kwamba Mungu atawapa ninyi nyote huduma kuu wakati tukiwa hapa pamoja kwenye Pwani hii ya Magharibi.

⁵ Ninataka kuwashukuru ndugu zangu hapa kwa ajili ya majaliwa haya makuu ya kudhamini mkutano hapa, kwa kuwa nilihisi kwamba, mara nyingine tena kabla ya kwenda ng'ambo, ingekuwa ni majaliwa makuu kwangu kuwatembelea marafiki zangu huku na huko Pwani hii ya Magharibi. Nasi tuko hapa usiku wa leo, katika Jina la Bwana Yesu, kuhudumu na kufanya yote tuwezayo kumsaidia kila mtu kumjua Yeye vizuri kuliko wanavyomjua sasa. Natumaini ya kwamba mkutano utakapokwisha nitamjua Yeye vizuri zaidi kuliko ninavyomjua sasa, maana kila siku sote tunaishi kwa kusudi hilo, kujaribu ku—kumjua Yeye vizuri zaidi kidogo.

⁶ Mwajua, mtu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikizungumza juu ya jambo fulani, na sarufi yangu ni mbaya sana kwa vyovyote vile, na kwa hiyo mimi... mtu fulani akasema, kwanza kabisa ilikuwa ni mwanatheolojia mashuhuri, akasema, “Kamwe huijui Biblia yako.”

7 Nikasema, “Lakini ninamjua Mwandishi wake vizuri sana.” Kwa hiyo, jambo ndilo hilo. “Kumjua Yeye ni Uzima.” Na kama Yeye ndiye Mwandishi wa Neno, Yeye daima atalithibitisha Neno Lake kwamba ni kweli, ninaamini hilo. Na kuna mengi ambayo Yeye anaweza kufanya, na hufanya ambayo hayaajaandikwa katika Biblia, lakini maadamu ninaliona likifunuliwa tu katika hizo kurasa, ni—ninahisi hilo (Ungeliitaje?), hakikisho hilo, mwajua, ya kwamba kila kitu kinaendelea vizuri, kwa sababu inaonekana tu kana kwamba kinapitia moja kwa moja kwenye hizo kurasa, kwa hiyo hilo linatufanya—linatufanya tujisikie vizuri zaidi.

8 Tuko njiani sasa kuelekea Anchorage, Alaska, kupanda Pwani ya Magharibi, kuanzia hapa California. Ndio kwanza tutoke Green Lake, Wisconsin, ambako Wafanyabiashara wa Full Gospel ambao, mara mbili za mwisho kuwa hapa nilikuwa pamoja nao, nasi tulikuwa na m—mkutano wa mkoa huko Green, naamini ilikuwa Green Lake, Wisconsin. Ndipo tukashuka kuja Chicago kwa ajili ya ushirika huko pamoja na Wakristo, tukawa na wakati mzuri sana, kusanyiko kubwa, watu wengi, na Bwana akatubariki pamoja katika jitihada zetu dhaifu za kujaribu kuwahudumia watu Wake.

9 Ndipo kutoka huko tukaenda, kutoka huko tukaelekea Pines Kusini, Carolina Kaskazini. Daima ninataka kuita hiyo Pines Kusini, inapaswa kuwa ni Carolina Kusini, lakini iko katika Carolina Kaskazini. Na bila shaka tulikuwa na wakati wa ushirika kule pamoja na mkutano wa Udugu wa Madhehebu Mbalimbali, wakati mzuri sana. Halafu basi, kutoka hapo tushuke tuingie, twende Carolina Kusini, hadi Columbia, na hapo tukakutana na watu, na tukijua ya kwamba tulikuwa tukija huku kwenye Pwani ya Magharibi. Wote walio wageni huko, kama tulivyo sisi sote, wasafiri wanaokiri tumaini hili kuu tulilo nalo katika Kristo.

10 Hatudai haya kuwa makazi yetu, sisi ni wasafiri na wageni, “Tunautafuta Mji, ambao Mwenye Kuujienga na Kuubuni ni Mungu.” Huo ulikuwa ndio msimamo wa Ibrahimu, alikuwa akiutafuta Mji. Nasi ni watoto wa Ibrahimu, tukiwa ndani ya Kristo, sisi ni Uzao wa Ibrahimu. Bila shaka tunajua ya kwamba Isaka alikuwa ni uzao wa kawaida, nao uzao wa kawaida wote uliutazamia Mji huo, ni zaidi sana vipi Uzao wa Kifalme unapaswa kuutafuta, Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu? Nami ninaamini Kanisa siku hizi, walioitwa watoke, ni Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu.

11 Tunakiri ya kwamba hapa si nyumbani kwetu, kwa kuwa hatuna nanga hapa duniani; na kama tunayo, natumaini tutaikatilia mbali upesi sana, ili kwamba kama Yeye angekuja usiku wa leo, tungetwaliwa juu, sio kutiwa nanga huku chini duniani.

¹² Ninashukuru sana kwa ajili ya fursa hii. Na sasa, najua inachelewa kidogo upesi sana, mengi sana ya kusemwa, inaonekana kana kwamba kuna muda mfupi sana wa kuyasema, lakini, inakufanya ki—kidogo kuwa na wasiwasi, kama ulimwengu mzima ulivyo na presha, wakijaribu kuharakisha na kufanya jambo fulani. Lakini ninatumaini ya kwamba hatutafanya hivyo wakati wa uamsho huu, kwamba tutakuwa tu kama tulivyokuwa muda mrefu uliopita, kidogo tu tukishusha presha, na kuachilia, na tuwe tu sisi wenyewe. . . ? . . . tuwe tu Wakristo na kushirikiana mmoja na mwenzake, huku Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ikitusafisha na uchafu wote.

¹³ Na sasa, nimekuja pia kutupa wavu wangu pamoja na hawa ndugu. Sasa, mnajua kila mmoja wetu ni wavuvi. Mnajua Bwa—Bwana alimwambia mvuvi wakati mmoja, Yeye alisema wamfuate na wawe wavuvi wa watu, na hao ndio walio hapa jukwaani usiku wa leo, ni wavuvi wa watu.

¹⁴ Tunasimama pembeni mahali fulani kanisani mwetu, tunatupa wavu kupitia ujirani wote, na kukusanyika pamoja na wote tuwezao, tukimleta ndani kila mwenye dhambi, haidhuru yuko mahali gani, tunajaribu kumleta kwa Kristo. Vema basi, unakuja wakati ambapo tunataka kufika mbali sana, kwa hiyo tunaunganisha nyavu zetu zote pamoja ili tuweze kwenda huko *mbali* sana na kuvua wengi sana. Na hilo ndilo lilituleta hapa usiku wa leo, nami niliunganisha tu wavu wangu katika ushirika wa upendo karibu na ndugu zangu, na wavu wao kuvua kwa juya huko *mbali* kupitia Los Angeles, na kote, tuone ni watu wangapi tunaoweza kupata kwa ajili ya Kristo, hilo ndilo kusudi la kuwa hapa.

¹⁵ Sasa, sisi, bila shaka, tunajua katika kuvua kwa juya unapata kila kitu kinachokuja, lakini kuna wengine kule ambao watakuwa ni samaki bila shaka kabisa, na Mungu atawachukua.

¹⁶ Sasa, niombeeni ninapozungumza, na kuwaombea wagonjwa. Nami si mponyaji, nimeitwa hivyo, bali mimi siye, mimi ni ndugu yenu, ndu—ndugu yenu tu hapa akiwaombea wagonjwa.

¹⁷ Na kwa hiyo, mimi, ninajua ya kwamba shuhuda hutoa msukumo mkubwa, na ninii tu, jambo fulani lilitukia usiku wa mwisho, ama, usiku uliotangulia wa mwisho huko Columbia, lilitoa taarifa nchini kule. Ninii. . . Wasingeweza kumwingiza maskini mtoto mchanga kwenye mstari wa maombi. Alikuwa ni mtoto mwenye kichwa kilichojawa maji, maskini uso wake mwembamba, na kichwa chake kimetokeza sana nje, alionekana kuwa na umri wa mwaka mmoja au miwili, nayo macho yake yameisha, mnajua jinsi yafanyavyo, na mishipa mikubwa kichwani mwake. Nao madaktari, matabibu wa duniani, ilibidi wamdunge sindano kila siku apate kuishi.

¹⁸ Nao wasingeweza kumwingiza huyo jamaa mdogo, kwa hiyo walikuwa wamemweka nyuma ya pazia, nami nikarudi nyuma kumwomba, kwa sababu wanawaomba wanapokuja na kadi za maombi, nao wanachukua kadi, nao wanazisambaza kila siku. Na kwa hiyo, naye maskini jamaa huyo hakuwa na kadi, naye mama yake asingeweza kukaa zaidi ya huo usiku mmoja, kwa hiyo tukamwomba maskini jamaa huyo nyuma ya jukwaa. Basi kesho yake asubuhi, lilikuwa ni jambo la kushangaza sana, mishipa hiyo yote mikubwa ilikuwa imetoweka, na maskini kichwa chake kidogo kilikuwa ni cha kawaida kabisa. Kwa hiyo wao—wao—wakampelekea daktari, bila kusema chochote, ndipo huyo tabibu akamwambia na kumchunguza, kitu fulani katika damu yake, iliwabidi kumdunga sindano hizi, naye akasema, “Huyu mtoto hahitaji sindano zozote.” Akasema, “Sijawahi kuona kitu kama hiki hapo awali.”

¹⁹ Na kwa hiyo, ilizusha tu uvumi mkubwa katika ujirani, na kama ilivyokuwa katika nyakati za Biblia, ilienea kila mahali, upendo na sifa za Bwana wetu Yesu, jinsi ambavyo angali anaweza kuwaponya wagonjwa, haidhuru ni kitu gani, Yeye angali anaweza kukiponya. Ni . . .

²⁰ Yeye ameninii—Yeye ameninii . . . Nguvu zimewekwa kwenye sanduku, Naye ametupatia kila mmoja Ufunguo, huo ni Jina Lake. Basi kama hatuogopi kuitia sahihi, mbona, bila shaka Yeye ataiidhini- . . . Hakika ataifanya hiyo hundi ikubalike ifikapo kule, iwapo ina Jina Lake nyuma yake. “Mwombeni Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya,” Yeye alisema, nami ninaamini hilo. Lolote mtakaloomba katika Jina Lake, mkiamini mnalipokea, mtalipokea.

²¹ Sasa, nafikiri kesho asubuhi ni kiamshakinywa cha wahudumu, nafikiri. Daima nina furaha kwa ajili ya hao, kuweza kukutana na ndugu zangu.

Nami ninatazamia kuwaona ninyi ndugu, kesho asubuhi, kwenye kiamshakinywa.

²² Nami nadhani ya kwamba Wafanyabiashara hapa, mbona, huenda watachukua a—asubuhi ya Jumamosi? Je, hiyo ni rasmi sasa? Jumamosi asubuhi, huko Clifton. Vema, nitapata zaidi ya huo uji mzuri walio nao huko chini basi, huo ni mzuri sana, na—naupenda huo. Kwa hiyo tutakuwa tukitazamia, huko juu, kuwaona huko juu.

²³ Sasa, maji mengi yamepitia kwenye bwawa hilo tangu ninii (Hilo ni tamshi la kusini.), tangu tulipokutana hapo awali. Nusura tuuawe, hivi majuzi, kwa kulipuka kwa bunduki. Mnaweza kuliona kote usoni mwangu, na, lakini Bwana aliyaokoa maisha yangu, nami ninashukuru kuwa hapa.

²⁴ Nilikuwa nikipiga bunduki iliyokuwa imetobolewa upya na Bw. Weatherby hapa juu, na nikapewa kuwa ni “sawa.” Nami nilikuwa nimepiga risasi mara kadhaa, nami nikaona

uvimbe kwenye ile duara, kisha nikaingiza risasi nyingine, nao bado hawajui kilichotukia, hiyo bunduki ikalipuka, na kuulipua mtutu yadi hamsini mbele yangu, na kuvilipua vipande vya bunduki kupitia kwenye miti, na yote niliyoona yalikuwa tu moto mwekundu ukiruka juu.

²⁵ Na wakati wao...Walidhani ningeninii...Bila shaka, vipande vilichomekwa kwenye fuvu la kichwa changu, na ninii tu, vipande kumi na vitano vikaingia tu chini ya macho yangu, na kimoja kikapitia *hapa* na kuvunja ncha ya jino, na kunikata usoni (Ndipo wakati wao...Sikujua mahali nilipokuwa kwa dakika chache, bila shaka, wala nisingeweza kuona, wala...), ni kama tu kwamba ulinirushia sambusa usoni mwangu, yapata majuma manne yaliyopita.

²⁶ Ninge vuta jicho *hili* juu, na kuona, kuangalia pande zote, nikamwona yule mtu aliyekuwa ameshuka kule chini pamoja nami kwenye uwanja wa shabaha, ambapo mimi hupiga shabaha hii, alikuwa akienda kwenye shabaha. Wala nisingeweza kusikia, nisingeweza kuongea, nisingeweza kusikia, wala kuona. Na hatimaye, nikapata usikivu wake, akaja pale juu, nami nikaikomesha damu kwa mkono wangu, nasi tukaomba, nayo damu ikakoma kabisa, nami nilikuwa nimelowa mwili mzima.

²⁷ Ndipo wakanipeleka kwa daktari, naye akasema, “Loo, jamani!” Ninasahau ni tani ngapi za presha wanasema bunduki hiyo ingestahimili. Kasema, “Wakati mtu huyo alipokuja na kukuona, alipaswa tu kuikuta miguu *hapa* chini, bila kichwa wala mabega, kukipasua chuma hicho ingeulipua mwili wote.” Nayo ilikuwa karibu tu *hivi* na jicho langu wakati ilipofyatuka, kwa hiyo ninashukuru kuwa hapa, ninashukuru sana.

²⁸ Naye tabibu aliyeangalia mahali hapo, alisema, “Vema, kuna moja tu...” Kasema, “Hakuna kitu kingaliweza kufanywa,” akasema, “kwa sababu hicho chuma kilirudi ndani kabisa kwenye jicho,” kisha kasema, “haikuligusa jicho.” Ndipo akasema, “Jambo pekee ninalojua ambalo, ninaweza kusema, hapana shaka Bwana mwema alikuwa ameketi kwenye benchi kumlinda mtumishi Wake asubuhi hiyo, la sivyo asingeninii...” Kwa hiyo naona ya kwamba—ya kwamba Yeye aliniweka hapa kuwahudumia, na kuwasaidia, nanyi mnisaidie, nasi sote tuko hapa pamoja kusaidiana.

²⁹ Na sasa, tunataka kuligeukia Neno Lake, ninalipenda tu Neno Lake. Na kidogo ni ninii...Sikuzote, kwenye usiku wa kwanza, tunachelewa kidogo kuanza, bali tunatumaini kuondoka kwa wakati ufaao. Nasi tutajaribu kuwaombea, kuna wagonjwa, Billy aliniambia alisambaza kadi. Na—na sasa, tuspowaingiza wote usiku wa leo, zishikilieni tu, tutazichukua, wala tusiwe na haraka.

³⁰ Na sasa hebu, kabla hatujasoma Neno Lake, hebu na tuzungumze na Yeye kwa dakika moja tu kwa maombi,

tunapoinamisha vichwa vyetu, nami ninatumaini ya kwamba mioyo yetu pia itainamishwa. Sasa, wakati mmeinamisha vichwa vyenu, macho yenu yamefumbwa, na moyo wako umeelekezwa kwa Mungu, sijui tu kama kuna haja zozote mngetaka zikumbukwe, inueni tu mikono yenu. Na kwa hilo mnasema, “Mungu, unajua kile ninachohitaji sasa, usiku wa leo.” Mungu awabariki, hilo ni jema.

³¹ Baba yetu wa Mbinguni, sasa tunakikaribia Kiti Chako cha neema, tusingetamani kusimama kwenye Kiti cha Enzi cha haki, kwa sababu tusingejisikia kwamba tungeweza kusimama pale, bali tunapokuja kwa njia ya neema, Wewe umetuagiza tuje. Nasi tuna furaha sana kwamba tuna majaliwa ya kukukaribia Wewe, Yehova Mkuu Mwenye Nguvu, katika njia ya neema ya Yesu Kristo.

³² Sasa, tunakuja katika Jina Lake, tukijua ya kwamba Yeye alisema kwamba, “Walipo wawili au zaidi wamekusanyika katika Jina Langu, basi nitakuwa katikati yao.” Na tena, Yeye alisema, “Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, mtapewa.” Nasi tuna hakikisho sasa, Bwana, ya kwamba kwa ahadi hizi za thamani za Neno la Mungu, ya kwamba Wewe uko hapa kusikiliza.

³³ Na, Baba, kwanza tungenesema, “Utusamehe makosa yetu, kama sisi nasi tunavyowasamehe wengine wanaotukosea.” Nasi tunaomba, Bwana, ya kwamba Wewe hutatutia majaribuni, bali utuokoe na yule mwovu. Pia jalia Ufalme wa Mungu utushukie na kubariki kukusanyika kwetu pamoja. Bariki kusomwa kwa Neno, na kufanya mambo yote, Bwana, kwa utukufu wa Ufalme Wako, kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

³⁴ Sasa, ninyi mnaopenda kwa namna fulani kuandika fungu dogo, ningetaka msome pamoja nami, usiku wa leo, katika Mathayo Mtakatifu 14, kuanzia kifungu cha 22, kwa dakika chache tu kama mtanivumilia.

Mara Yesu akawalazimisha wanafunzi wake wapande chomboni, na kutangulia mbele yake kwenda ng'ambo, wakati yeye alipokuwa akiwaaga makutano.

Naye alipotaka...alipokwisha kuwaaga makutano, alipanda mlimani faraghani, kwenda kuomba: na kulipokuwa jioni, alikuwako huko peke yake.

Na kile chombo kimekwisha kufika katikati ya bahari, kinataabika sana na mawimbi, maana upepo ulikuwa wa mbisho.

Hata wakati wa zamu ya nne ya usiku Yesu akawaenda, akienda kwa miguu juu ya bahari.

...wanafunzi walipomwona akitembea juu ya bahari wakafadhaika, wakisema, Ni kivuli; wakapiga youwe kwa hofu.

Mara Yesu . . . Mara Yesu alinena, akawaambia, Jipeni moyo; ni mimi; msioCOPE.

³⁵ Ninataka kuutumia huu, usiku wa leo, kama namna ya mkutano wa ushuhuda.

³⁶ Hapana shaka ilikuwa karibu wakati jua lilipokuwa likitua, na ilikuwa ni siku mbaya sana, kungekuwa, kulikuwa na shughuli nyingi katika ibada siku hiyo, walikuwa wameona mambo makubwa mno yakitendeka. Mnajua, wakati unapokuwa Mbele za Kristo, daima unaona mambo ya kimiujiza yakitendeka, hiyo ndiyo sababu ninapenda kuishi katika Uwepo Wake, ni kuona mkono Wake mkuu, mpole ukienda kuhudumu. Ningalipenda kuwa nikitembea pamoja Naye siku hizo.

³⁷ Lakini nafikiri, siku hizi, labda ni majaliwa makubwa zaidi, kwa sababu Yeye anatembea ndani yetu. Wakati huo Yeye alikuwa nje akielekeza, sasa Yeye yuko ndani akijielekeza Mwenyewe yale anayofanya, nami nina furaha sana kwa ajili ya majaliwa hayo.

³⁸ Sasa, ninii, ningefikiri, labda, ilikuwa ni mmoja wa watu wakubwa zaidi wa kundi hilo, tungemwita Simoni, labda, ambaye alikuwa mmoja wa waongofu kwa Bwana Yesu, aliyekuwa akiusukuma mtumbwi kutoka ukingoni, ambapo walikuwa wameiegesha baada ya kusafiri na kuhubiri pwani. Na—nayo hiyo siku ingalikuwa na joto, alikuwa amechoka, ndipo akausukuma mtumbwi majini, akaingia ndani, akaketi karibu na ndugu yake, Andrea, akachukua makasia katika maskini meli hiyo.

³⁹ Sasa, meli za siku hizo hazikuwa kama meli za siku hizi, hazikuendeshwa na jeti, ama—ama kwa nguvu za umeme, zilivutwa kwa mkono; nyingi yazo, kwa namna fulani ni kama mtumbwi wa—wa—wa mvuvi siku hizi. Zilikuwa na makasia marefu, na kungekuwako na mtu upande mmoja mwenye kasia, moja kwa moja kando yake kungekuwako na mtu mwingine. Ndipo walikuwa na tanga, wakati upepo ulipokuwa sawa, wangeinua tanga hili juu, na kuunasa upepo, na—nao ungewapulizia hadi mahali pao, kikomo, ambako walikuwa wamekusudia kwenda. Ndipo basi kama upepo haukuwa mzuri sana, wangechukua makasia, ndipo kungekuwa na watu wawili katika kila kiti wakivuta makasia.

⁴⁰ Nami ninaweza kumwona Simoni wakati akipanda chomboni, jamaa mkubwa, mwenye nguvu, labda mwenye upara, naye akaketi karibu na, ndugu yake Andrea, akachukua makasia, halafu wanapiga mapigo kadhaa, kisha wanawapungia mkono, nao watu wamesimama ukingoni wakiwapungia mikono. Onyesho la kuvutia sana, kwa sababu walikuwa wakiwaalika, “Rudini.”

⁴¹ Kuna jambo fulani, mwajua, unapokutana na watu ambao mna mambo shirika, mazungumzo yenu ni mambo, ushirika

wenu basi unakuwa mzuri sana, wakati mnapoweza kuwa na mambo shirika. Hiyo ndiyo sababu tuko hapa usiku wa leo, kwa sababu tuna mambo shirika, tunapenda kuzungumza sisi kwa sisi, tunazungumza juu ya mambo yale yale.

⁴² Na hivyo ndivyo walivyokuwa, walikuwa wakizungumza siku hiyo, na, juu ya Mungu, na kuhusu uweza Wake mkuu, na kuona nguvu Zake zikitenda kazi miongoni mwao. Nao mkutano ulikuwa umekwisha, nao walikuwa wakienda nyumbani, ama, ng'ambo ya ziwa kwa ajili ya kampeni iliyofuata. Nami ninaweza kuwazia jinsi mioyo yao ilivyojisikia walipokuwa wakiwapungia mikono kuwaaga hao watu wa thamani wa siku hiyo, baada ya kushiriki katika kazi kuu za Kristo.

⁴³ Sasa, ni wakati uliobarikiwa jinsi gani, jinsi mnavyochukua kuachana! Ni upendo ambao, unatokea moyoni. Ni vibaya sana kwamba mengi ya hayo hayapo siku hizi katika makusanyiko yetu, ni ule upendo halisi ambao Kanisa linapaswa kuwa nao mmoja kwa mwingine.

⁴⁴ Katika siku za mwanzoni za huduma yangu, nilikuwa mchungaji wa kanisa, nasi tulikuwa tukikusanyika usiku, kwa njia ndogo ya kinyumbani, na kuweka mikono yetu pamoja, nasi tungeimba wimbo huo:

Kibarikiwe kifungo kifungacho
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa watu wenye nia moja
Ni kama ule wa huko juu.

Tunapoachana,
Inatupa maumivu ya ndani;
Lakini bado tutakuwa tumeungana moyoni,
Na kutumaini kukutana tena.

⁴⁵ Nyingi za maskini nyuso hizo za kale za thamani tayari zipo Mbele za Mungu, nao wimbo huo ungali unatoa mwangwi nafsini mwangu, kwamba "bado tutakuwa tumeungana moyoni, na kutumainia kukutana tena." Nimesaidia kuweka mawe ya makaburi juu ya mengi ya makaburi yao, na kuwaona wakitupa tena mavumbi ndani wakati nilipourudisha huo mwili, "majivu kwa majivu na mavumbi kwa mavumbi," lakini, "U mavumbi wewe, mavumbini utarudi, halikunewa juu ya nafsi." Hiyo ni kweli, imeenda kwenye Uwepo wa Mungu, ushirika huo, kitu ambacho . . .

⁴⁶ Ndugu wahudumu wangeingia na kusema, "Inafanywaje, Ndugu Branham?" Tungeninii, ni vigumu tu kuachana, tulitaka tu kupeana mikono tena, na wakati mwingine tungenda tu kwenye gari, na kupiganapigana mabegani, sio kama kwa kujifanya, kuigiza, bali kitu ambacho kweli kilikuwa kinatoka mioyoni mwetu.

⁴⁷ Laiti tu Kanisa lote la Mungu aliye hai lingeweza kujisikia hivyo kulihusu usiku wa leo, tungekuwa tu katika umoja

mzuri sana kwa ajili ya kuja kwa Bwana, ambako ninaamini kumekaribia sasa, ninaamini tunaishi katika vivuli vyake hasa.

⁴⁸ Na asipokuja leo, nitakuwa nikimtazamia kesho, na asipokuja mwaka huu, nitakuwa nikimtazamia mwaka ujao. Wakati wowote tu, ninataka kukutazamia kuja Kwake kila dakika, nikiendelea, nikifanya tu yale niwezayo, lakini ningali nikiamini ya kwamba Yeye yuaja wakati wowote, nikijiandaa kwa ajili yake. Nami nafikiri maandalizi ya Kanisa yanapaswa kusimama katika hadhi hiyo wakati wote, kwamba bila shaka tunapaswa kuwa tukikutazamia Kuja kwa Bwana.

⁴⁹ Na sasa, kwa kuwa ushirika mzuri sana ulikuwa umefurahiwa, wanafunzi hawa wakienda zao baharini sasa, ama, wakivuka ziwa, ningewazia jua lilitua kama lilivyotua alasiri ya leo, nzuri huko nje ng'ambo ya bahari. Nayo maji yalikuwa shwari nao wangepanya mapigo kadhaa kwa makasia yao, kisha wanasimama, na kuwapungia mkono wa kwaheri, na hao kwenye ukingo wakiwaaga kwaheri, "Rudini, mkatuone tena."

⁵⁰ Na—na wakati ule mtumbwi mdogo ulipoondoka, umati wa watu wakipunga mkono uliendelea kufifia zaidi na zaidi, hata hatimaye wakatoweka. Huenda walivuta kwa muda mrefu, na—na kutoa jasho kidogo, mwajua, unapovuta makasia hayo makubwa, mazito. Wengi wenu ninyi watu ambao mmevuta mashua mnajua hilo linamaanisha nini.

⁵¹ Na baada ya wao . . . hapana shaka ilikuwa ni kijana Yohana ambaye kwa namna fulani alichoka kwanza, mwajua, akiwa jamaa mdogo, huenda alisimama na kupangusa jasho kutoka kwenye paji la uso wake, kasema, "Mnasemaje, ndugu? Hebu tusimame kwa dakika chache tuvute pumzi kidogo," wakati wao, vema, akiwa kijana, na kwa hiyo wakavuta makasia yao ndani.

⁵² Baada ya kusafiri kidogo alisema, "Mbona tusiwe na mkutano wa ushuhuda tunapongojea hapa, kupumzika kidogo?" Ba—basi mwajua, kwa namna fulani, unapokuwa na mambo mengi moyoni mwako, wala huwezi kuyanyamazia, huna budi kusema jambo fulani kuyahusu. Na kwa hiyo ningewazia jamaa huyo mdogo, kitu fulani tu kikichemka ndani yake, alikuwa ameona kitu siku hiyo kilichomshawishi. Na mtu wakati ameshawishika kabisa na jambo lolote, hawezi kutulia, hivyo tu, hana budi tu kufanya jambo fulani kulihusu.

⁵³ Ndipo wakati Kanisa linaposhawishika kabisa ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, ya kwamba Yeye yupo hapa pamoja nasi, leo, katika umbo la Roho, ninawaambia, kutakuwako na uamsho utakaoipiga nchi hii ambao utalitia moto taifa, wakati wafuasi wote wa Kanisa wameshawishika kabisa. Lakini inawabidi kushawishika kwanza, kabla hawajaweza kuwa waaminifu kwake.

54 Kwa hiyo kijana Yohana akasema, “Tutaanzisha mkutano wa ushuhuda huku tuingojea, ningependa kuwa wa kwanza kushuhudia,” maana ilikuwa tu inawaka ndani yake.

55 Ninakumbuka dada fulani aliyekuwa kanisani mwetu, angeimba wimbo mdogo, kitu fulani nasahau ni kipi, jinsi yeye, mnavyokiita, lakini *kitu fulani*, “Kukimbia, kukimbia, kukimbia, wala huwezi kutulia,” ama kitu kama hicho, “nimefika tu, wala siwezi kutulia,” ama kitu fulani. Lakini alikuwa, bila shaka alikuwa na yu—yubile halisi kwake pekee, kama hao wengine walikuwa nayo au la, alikuwa na wakati mzuri sana nayo. Kwa hiyo, hiyo hapana shaka ilikuwa ndiyo hali ambayo Yohana alikuwa nayo. Na hebu tusimame tu sasa, na kuwasikiliza wakishuhudia.

56 Yohana akasema, “Ndugu, kuna jambo moja ambalo nimeshawishika nalo kabisa, tunaweza kuuambia ulimwengu, tangu leo na kuendelea, ya kwamba hatufuati namna fulani ya bingwatapeli, hatumfuati nabii fulani wa uongo, kitu fulani chenye *kiburi* ambacho—ambacho hakijui chochote, bali tunamfuata Mungu, hatumfuati nabii fulani wa uongo.

57 “Ninaweza kukumbuka zile siku nilipokuwa mvulana mdogo, nilizoea kucheza kwenye majira ya kuchipua kando ya vilima, nami ninamkumbuka mama yangu mrembo wa Kiyahudi, alikuwa akiniita ndani, na—na kuniweka kwenye baraza lililoangalia upande wa Yordani, anipembeze mpaka nilale mikononi mwake, naye angenisimulia hadithi za Biblia. Kisha angenionyesha ambapo Yoshua, yule shujaa mkuu, alivuka huo mto chini ya nguvu za Yehova, akayafingirisha hayo maji nyuma, na katika hayo majira ya kuchipua mafuriko makubwa yenye matope yakasimama kimya, wakati watu wetu wakivuka kuingia kwenye ardhi yao wenyewe katika nchi yao wenyewe, wakati wangukuja kutoka kwa watumwa kutoka nchi nyingine, walikuwa huko chini wakiishi kama watumwa, na sasa walikuwa wameletwa katika nchi yao wenyewe.

58 “Naye akaniambia jinsi ambavyo Mungu aliwajalia katika safari yao, jinsi ambavyo kwa miaka arobaini huko nje nyikani, bila kukosa hata wakati mmoja, Mungu alishusha mkate kutoka mbinguni juu ya nchi kila usiku ili wapate kuupata mpya kila siku.

59 “Nami nilikuwa nikisema kama mvulana mdogo, ‘Mama, ni jambo la ajabu, sielewi jinsi Mungu anavyofanya hivyo. Je, Yeye ana zamu ya usiku inayofanya kazi huko juu, nazo mbingu zote zimejaa matanuru ya mikate ambapo Yeye huoka mikate, nao Malaika wanaioka, kisha wanashuka kwa ngazi na kuitandaza kote ardhini kwa ajili ya watoto Wake?’ Nakumbuka ningemwuliza Mama hivyo.

60 “Naye angeniambia, ‘Maskini mvulana wangu, Yohana, bila shaka unaelewa kama mtoto, lakini unajua, haimbidi

Yehova kufanya mambo ya namna hiyo, Yehova ni Muumba, haimlazimu kuwa na meko, na kuoka mkate, na kufuata utaratibu tunaofuata, bali Yeye ni Muumba, na yote anayopaswa kufanya ni kunena tu Neno mkate ukawa.’

⁶¹ “Na ndugu, leo wakati—wakati Andrea aliposhuka kwenda kule na kuchukua biskuti hizo tano kutoka kwa mvulana huyo mdogo aliyekuwa ametoroka shuleni, na kutupa chakula hicho cha mchana, basi nilipomwona Yeye akiuchukua mkate huo, na kuumega, na kuwalisha watu elfu tano, nilijua huyo hakuwa nabii wa uongo, kuna uhusiano fulani hapo na Mungu, kwa sababu Mungu pekee ndiye anayeweza kufanya hivyo, Huyo hapana shaka, alikuwa ni Mungu. Na hivi mliona, Yeye alionekana tu kama Yehova wakati aliposimama pale akiumega mkate huo?”

⁶² “Nanyi mnajua, nilinyemelea nyuma ya ule mwamba, nikapanda juu, na kuangalia kule, nami nikasema, ‘Sijui anaipata wapi?’ Naye akaichukua biskuti hii, ndipo alipoimega ile biskuti, basi niliangalia nchani mwake, ndipo akampa mmoja wenu ninyi ndugu, wakati mkono Wake ulipoanza kurudi, kulikuwa na biskuti ile ile tena, nzima. Kwa hiyo ha—haikumbidi ku—kuioka tena, iliumbika moja kwa moja mkononi Mwake. Kwa hiyo hapana shaka ilikuwa ni Yehova, na, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Muumba, niliona jinsi alivyotenda, ilikuwa ni Yehova, ninajua Ndiye. Naye si kitu cha uongo, nami nimeshawishika kabisa. Naye mvulana huyo mdogo, jinsi nilivyoyaona macho yake madogo wakati alipoangalia juu.”

⁶³ Sasa, mnaona, kwa wavulana wadogo hapa usiku wa leo, maskini mvulana huyo alikuwa akienda, labda akienda kuvua samaki, ama huenda alikuwa akienda zake shuleni, lakini wakati yeye—wakati alipoona umati huo, yeye, kama mvulana yeyote mdogo, a—alikingia kama mtazamaji aone kilichokuwa kikiendelea. Lakini mara aliposikia Sauti ya Yesu, hiyo—hiyo ilikuwa ni bora kuliko kwenda kuvua samaki, a—alitaka kusikiliza, Yale yaliyosemwa.

⁶⁴ Ndipo wakauliza kama kulikuwa na chakula, naye alikuwa tu na samaki wake wawili wadogo na biskuti tano. Na kwa hiyo basi, ha—hakikuwa kingi sana mkononi mwa mvulana huyo mdogo, bali alipomwacha Yesu akichukue, angalia yale kiliyofanya. Na sasa, hivyo ndivyo ilivyo, maisha yetu hayana faida sana maadamu tunayashughulikia sisi wenyewe, lakini mara yakiwa mikononi mwa Muumba, jinsi anavyoweza kuchukua kile kidogo tulicho nacho, na kukisukuma, na kuulisha umati, nanyi kumbukeni tu hilo. Unapomsikia Yesu akinena moyoni mwako, toa tu yote uliyo nayo Kwake, ndipo atanza kuyazidisha na kuwalisha wengine kwa ushuhuda wako, na chochote ulicho nacho cha kumpa, Yeye atakibariki.

⁶⁵ Kwa hiyo wakati Yohana alipomaliza ushuhuda wake, hata

kabla hajaketi, mvuvi huyu mashuhuri, mwenye misuli migumu, jina lake Petro, alisimama chomboni, akamwangalia Andrea, na kusema, “Ninakumbuka wakati ndugu yangu, Andrea, alipoenda kumsikiliza Yohana, aliniambia ya kwamba alikuwa akizungumza juu ya kuja kwa Masihi, kwa hiyo nilifikiri ilikuwa ni uvumi mwingine tu unaoenezwa nchini, ni mtu fulani tu, kwa kuwa walikuwa wakija na kuenda.

⁶⁶ “Kwa hiyo mnajua, Andrea alikuja siku moja akiwa ameshawishika kabisa ya kwamba Huyu alikuwa ndiye Masihi, kwa hiyo akaniita niende pamoja naye huko chini kumsikiliza Yeye asubuhi moja. Kwa hiyo nikamwambia ningenda kusikia mara moja, kwa sababu nilikuwa nimekata kauli niani mwangu ya kwamba kama alikuwa ndiye Masihi ningemjua, kwa sababu singemwendea kwa wazo lolote la kijinga, ningeiendea, hiyo hoja, kwa Maandiko, na ilibidi iwe kwa Biblia.

⁶⁷ “Naye Andrea hapa, ndugu yangu, anaweza kumkumbuka vizuri maskini baba yetu mwenye mvi, wakati aliponiketisha chomboni siku moja, baada ya sisi, karibu tuishiwe na chakula nyumbani, nalo pipa lilikuwa karibu tupu, na chupa imekauka, wala tusingeweza kukamata samaki yeyote, basi asubuhi hiyo, tulipokuwa tumekusanyika, tulikuwa na madeni ya kulipa, nasi tukaomba, ‘Mungu tupe samaki wengi leo.’ Nawe Andrea, unajua jinsi tulivyoyaombea mambo hayo, na jinsi Baba alivyotufundisha, ndipo siku hiyo tukapata samaki wengi sana, wa kutosha kulipia madeni yote, na kutupa chakula cha siku hiyo.

⁶⁸ “Siku hiyo Baba akanishika mkono, naye akasema, ‘Simoni, mvulana wangu, nimekufundisha mambo yaliyo sahihi. Siku zangu zote nimetamani kumwona huyo Masihi ajaye, ni—niliamini ya kwamba ningemwona, lakini inaonekana sasa kwamba mimi ni mzee, nami, labda sitaweza kumwona, na, lakini labda wewe utamwona katika siku zako. Tumemtazamia, katika vizazi vijavyo tangu mwanzo kabisa wa wakati, lakini siku moja, Simoni, Yeye atawasili, na asipokuja katika kizazi changu, anaweza akaja katika chako, kwa sababu Yeye ni ahadi ya Mungu.’”

⁶⁹ Ninapenda hilo. Ahadi ya Mungu haiwezi kushindwa. Hiyo ni kweli. Neno ni hakika, haliwezi kubadilika, halina budi kudumu jinsi tu lilivyoandikwa. Mungu atauhukumu ulimwengu siku moja, nao ulimwengu itabidi uwe na Kigezo. Na kama kanisa ndilo Kigezo, ni lipi, liko wapi kanisa hilo? Kuna mamia ya madhehebu mbalimbali ya hayo. Lakini Kigezo ambacho Mungu atauhukumia ni kwa Neno Lake.

⁷⁰ Ninaamini Neno, kwa kuwa katika Kitabu cha Ufunuo imeandikwa, “Yeyote atakayeongeza kitu kimoja kwake, au kuondoa lolote, huyo ataondolewa katika sehemu ya Kitabu cha

Uzima, kwake.” Kwa hiyo ninaamini ya kwamba Neno hili liko tu jinsi lilivyo. Ni Neno la Mungu tu.

71 Nami nitamfanya maskini Mfarisayo huyu mashuhuri usiku wa leo, aamini jambo lilo hilo wakati aliposema, “Simoni, kutakuwa na kila namna ya mambo ya uongo yatakayoinuka kote katika nyakati, ukiishi kuwa mzee, natumaini, lakini Masihi huyo atakapokuja, Simoni, nitakuambia kile atakachokuwa: Atakuwa vile vile hasa Maandiko yasemavyo Yeye atakuwa.

72 “Sasa, Musa, nabii wetu, ametwambia, katika Gombo letu katika Kumbukumbu la Torati, kwamba “Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kutoka miongoni mwenu kama nilivyo mimi.” Sasa, Simoni, utamjua kwa sababu atakuwa ni nabii. Nawe utakuwa . . . utamtambua kwa hilo, kwa sababu Maandiko yanasema hana budi kuwa ni nabii.

73 “Kwa hiyo mtaona mambo mengi yakiendelea, lakini Mtu huyu atakuwa ni nabii, na isitoshe, sisi Wayahudi tunajua ya kwamba Neno la Mungu humjia nabii” (Hivyo ndivyo Maandiko yasemavyo hasa, “Neno la Bwana liliwajia manabii.” Na kwa hiyo huyo—huyo Nabii alikuwa aje.). “sasa, usisahau hilo, Simoni,” aliniambia, na karibu katika maneno yake ya kufa aliniambia, ‘Mwanangu, usisahau, kumbuka, atakapowasili, atakuwa ni Nabii kama Musa, kwa sababu hivyo ndivyo inavyosema hasa.

74 “Na jinsi mtakavyojua Yeye atakuwa ni nabii, kwa sababu Musa ametwambia, nayo Maandiko yanatwambia, kwamba kama kuna mtu miongoni mwenu ambaye ni wa kiroho ama nabii, na yale asemayo yanatimia, basi msikieni. Lakini yasipotimia, basi msimwogope, kwa maana Neno la Bwana haliko pamoja naye, kwa sababu Mungu hawezi kusema uongo, Mungu hana budi kuwa Mkweli. Na kama Mtu huyo akiyasema, nayo yanatimia, basi hai—haikuwa ni huyo mtu, ilikuwa ni Mungu. Na kwa hiyo, hivyo ndivyo utakavyomjua Yeye.’

75 “Nanyi mnajua, niliposhuka kwenda siku hiyo, kwa namna fulani nilimshuku Andrea,” nami ninawazia akitikisa mabega yake namna *hiyo*. Kasema, “Kwa namna fulani nilimshuku ndugu yangu Andrea, nilifikiri ilikuwa tu ni kitu kingine. Lakini nilipoenda mkutanoni asubuhi hiyo, Andrea alikuwa amefika huko mapema sana kuliko mimi, kwa sababu ilinibidi kumalizana na zile nyavu, kutengeneza nyavu, basi nilipofika Mbele za Yesu wa Nazareti, aliniangalia moja kwa moja, Naye akasema, ‘Jina lako ni Simoni, nawe ni Mwana wa Yona.’

76 “Si kwamba tu alijua mimi ni nani, alimjua maskini yule baba yangu mtauwa.” Akasema, “Hilo lilitosha kwangu, nilijua papo hapo kwamba Huyu alikuwa Ndiye, Huyu alikuwa ndiye Nabii ambaye Musa alikuwa amenena habari zake, hiyo ilinishawishi kwamba alikuwa Ndiye.”

⁷⁷ Hata kabla ya kumaliza kuzungumza, Filipino akaruka na kusema, “Hebu kidogo, ndugu zangu. Loo, siwezi kujizuia zaidi!” Ndipo akageuka, akaangalia mbele ya hicho chombo, na kusema, “Nathanaeli, utanisamehe?”

“Mbona, hakika, Ndugu Filipino, ni majaliwa tu kwako, kukusikia ukishuhudia.”

⁷⁸ “Sasa, mimi na Nathanaeli tulikuwa wavulana pamoja. Tulikua, tulihudhuria sinagogi lile lile, tukaketi kwenye viti vile vile, tu—tulikuwa—tulikuwa wavulana pamoja, na sote wawili tulisoma Maandiko dhahiri sana. Nilikuwa nimesimama pale siku hiyo nilipomwona na kumsikia akimwambia Simoni kuhusu baba yake na habari zake. Nami nilisisimkwa sana, na sote wawili tulikuwa tumekubaliana ya kwamba Masihi ajapo, ilibidi Yeye awe ni Masihi wa Kimaandiko, ilibidi awe Masihi wa Kimaandiko. Kwa hiyo nikaondoka mbio haraka nilivyoweza.

⁷⁹ “Na—naye Nathanaeli, kamwe sisahau ile asubuhi nilipobisha mlangoni kule, karibu nilikuwa nimekimbia usiku na mchana kufika kule, nami nikabisha mlango, ndipo mke wako akasema, ‘Yuko nje kwenye kijisitu chake.’

⁸⁰ “Nami nikaenda huko nje, nawe ulikuwa ukiomba, nami nikakusikia katika maombi yako ukisema, ‘Ee Mungu, tumengojea muda mrefu sana, bali tunaamini ya kwamba ile saa itakaribia ambapo tutamwona yule Mkombozi, tunamtazamia wakati wowote. Na, Mungu, niko hapa asubuhi ya leo kwa sababu jambo la ajabu lilinipata jana jioni, niliota ndoto kwamba nilimwona. Nami ni—niko hapa asubuhi ya leo nikiomba.’”

⁸¹ Na mara aliposimama, vema, Filipino akasema, “Njoo, umwone Yule tuliye mwona, Masihi. Tumemwona Yeye aliyenenwa na Musa na manabii, Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusufu.” Hakusimama kuuliza jinsi hilo shamba la matunda lilivyokuwa likiendelea, ninii... alishawishika kabisa. Hiyo ndiyo shida siku hizi, tuna vitu vingine vingi sana ambavyo tunabeba, hata inaonekana kana kwamba hatujashawishika kabisa. Kwa hiyo kama tumeshawishika ni kweli, tulikabili moja kwa moja, tuliamini.

⁸² “Loo, nimekuja kwenye mkutano wa Ndugu Roberts, nitaombewa, kama nikiukosa hapo, nitaenda kwenye mkutano wa Ndugu Allen, kama nikiukosa huko, nitaenda kwenye mkutano wa Ndugu Branham” ama ninii... Usifanye hivyo. Shawishika ya kwamba Yeye ni Mungu, na uliamini, ya kwamba Neno Lake ni kweli, na ulitatie papo hapo, umeridhika kabisa. Hakuna kitu ndani yetu wanadamu, sisi ni wanadamu, ni: Yeye Ndiye aliyekufa, Yeye Ndiye, naam, aliyefufuka tena, na yu hai hata milele. Sisi ni viumbe vinavyopatikana na mauti, wawakilishi Wake, tu—tunakufa, wanadamu, bali Yeye hawezi kufa, Yeye ni Yule asiyepatikana na mauti.

83 Sasa, naye Filipino akaenda moja kwa moja kwenye hoja hiyo na kusema, “Njoo, umwone Yeye. Tulimwona.”

84 “Nawe Nathanaeli, unakumbuka ile hali ya kupanda kwa joto la mwili ghafla kulikokupitia? Uliwaza, kwani nimepatwa na nini? Hakika nilikuwa nimeingia wazimu mahali fulani. Mbona, ulisema, ‘Filipo, kwani umepatwa na nini? Mbona, kama Masihi angekuja, angetembea moja kwa moja kwenye ushoroba wa Mbinguni, ashuke moja kwa moja kwenye kundi le—letu wenyewe, Naye angelilizungumzia moja kwa moja kundi letu wenyewe la Mafarisayo, na Masadukayo, wala asiwakaribie kabisa. Kwa hiyo kusingekuwa na kitu kingine kwake. Vema, Naye angekuja moja kwa moja hekaluni kwenye makao makuu, na—na hapo angejitambulisha Mwenyewe kwa Kayafa, kuhani wetu mkuu, na hilo lingetosha.”

85 Lakini mnajua, Mungu hufanya mambo kwa njia Yake Mwenyewe. Yeye ananinii tu, ana njia ya kufanya jambo hilo. Yeye daima ana mambo kama hayo, afanyayo Yeye, ambayo Yeye... Yeye ni Mungu, na Yeye—Yeye hufanya kazi kama Mungu, Yeye—Yeye hutumika kama Mungu, kwa sababu Yeye ni asiyeapatikana na mauti, asiye na kikomo. Maskini akili zetu zenye kikomo zinawezaje kamwe kuifikia hiyo nia ya Mungu isiyu na kikomo? Loo, Yeye yuko kila mahali, anajua yote, Yeye ni—Yeye ni Mungu.

86 Na hapo, wakati... Yeye alisema, “Sikupoteza maneno yoyote kwa—kwa Nathanaeli, nilisema, ‘Njoo uone.’”

87 Hilo ni wazo zuri. Mnaona? Usikae nyumbani na kukosoa, njoo ujionee mwenyewe, hiyo ndiyo njia bora zaidi. “Yachunguzeni Maandiko,” Yesu alisema, “kwa kuwa ndani Yake mnadhani kwamba Yana... mna Uzima wa milele, na Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi.” Kwa maneno mengine, “Ni—nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Lakini nikizitenda hizo kazi, nanyi hamwezi kuniamini Mimi, ziaminini hizo kazi,” kwa kuwa kazi ndizo zinazoushuhudia ule ushuhuda. Unaweza *ushuhuda*, lakini kazi unazofanya, na maisha unayoishi yananena kwa sauti kubwa kuliko ushuhuda wote ambao ungeweza kutoa. Kwa hiyo kazi zinanena kwa sauti kubwa kuliko ushuhuda.

88 Akasema, “Ziaminini kazi nizifanyazo. Na nisipozitenda kazi za Mungu, basi msiniamini Mimi. Lakini kama nikizitenda hizo kazi, basi kama hamwezi kuniamini Mimi kuwa ni Mungu, basi aminini kazi nizifanyazo.” Sasa, angalieni, Yeye kamwe hakujitwalia Mwenyewe sifa, Yeye alisema, “Si Mimi, ni Baba anayekaa ndani Yangu, Yeye huzifanya hizo kazi.”

89 Sasa, tunaona ya kwamba Nathanaeli, akitembea ukingoni pamoja—pamoja na Filipino, na, mwajua, huenda Filipino alianzisha ushuhuda kama huu: akasema, “Je, unamkumbuka yule Simoni, yule mvuvi, yule mtu asiye na elimu yoyote?”

“Naam, nakumbu- . . . Nilimjua baba yake, Yona, naam.”

“Unakumbuka ulinunua samaki kutoka kwake wakati mmoja, asingeweza kutia sahihi ile risiti?”

“Naam, ninakumbuka hilo vizuri.”

⁹⁰ “Vema, Andrea, ndugu yake, alikuwa mwaminio wa Masihi naye akamwambia, kama vile mimi na wewe tumefundisha, ya kwamba Masihi atakuwa ni Nabii kama Musa, hiyo ndiyo njia ya Kimaandiko ya kumwendea Yeye. Na sasa, kama ni Yeye, basi haya ndiyo yaliyotukia: Wakati alipokuja Mbele za Yesu wa Nazareti, Yesu alimwambia yeye alikuwa ni nani, kasema, ‘Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.’ Nawe unajua nini, Nathanaeli? Haingenishangaza kama Yeye hakuwambia wewe ni nani utakapokuja. Huh-uh. Haitanishangaza.

⁹¹ “Nathanaeli akasema, ‘Vema, Filipino, sitakuwa mkosoaji, nitajionea tu.’ Vema, tulipofika mkutanoni,” huenda kulikuwa na mstari wa maombi, ama huenda walikuwa wameketi nje kwenye kusanyiko, ama popote pale, ama wakisimama, kwa namna fulani kulikuwa na kundi la Mafarisayo pale, nao walijua . . .

⁹² Sasa, walikuwa ni waethodoksi, bali hawakuamini katika mambo ya kimbinguni. Kwa hiyo wao—wao, wakisimama huku wameweka mikono yao nyuma yao, nao wakamwona Yesu akifanya ishara hizi, nao walijua ingewabidi kuwajibika kwa kusanyiko lao. Nao wasingeweza kusema halikufanywa, kwa sababu ilikuwa moja kwa moja mbele ya kusanyiko, kwa hiyo wakasema, “Yeye ni Beelzebuli. Yeye ni mkuu wa pepo. Hivyo ndivyo yeye. . . .” Kwa maneno mengine, pepo mchafu akifanya hivyo, ibilisi, mpiga ramli, ama pepo mwingine mchafu. Sote tunajua kwamba upiga ramli na upuuzi huo ni wa ibilisi. Na kwa hiyo walimwita Roho aliyekuwa ndani ya Kristo pepo mchafu.

⁹³ Naye akawaambia, kasema, “Ninawasamehe hilo, lakini siku moja Roho Mtakatifu yuaja, Yeye atafanya jambo lilo hilo, na kunena neno dhidi ya Huyo halitasamehewa kamwe katika ulimwengu huu, wala Ulimwengu ujao.” Kwa hiyo unashangaa kama tunaweza kuwa tunaishi katika siku hiyo?

⁹⁴ Kwa vyovyote vile, tunaona ya kwamba walipokuja kwenye, mahali watu walipokuwa, Yesu aliangalia moja kwa moja kwenye huo umati, ama labda huenda Nathanaeli aliingia mstarini mahali fulani, naye Yesu akamtazama na kusema, “Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!” Kamwe hakumwambia yeye alikuwa ni nani, bali alisema, “Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake.”

⁹⁵ Akasema, “Rabi,” (ambalo linamaanisha “mwalimu, bwana,”) “ulipata kunijua lini?” (“Sasa, mimi ni mgeni Kwako,” kwa maneno mengine.) “Ulipata kunijua lini?”

Na hapa laja swa-...hili hapa linarudi, Yeye akasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti nilikuona.” Loo, jamani!

⁹⁶ Ninaweza kuwazia maskini Nathanaeli akisimama mbele ya hicho chombo, na kumpa mikono, na kupaza sauti kidogo, na kucheza-cheza karibu na huo mtumbwi, na huenda ilikuwa ni Mathayo aliyesema, “Tulieni, mtakipindua hiki chombo.” Loo, walikuwa wakiamka na kuwa na hizo yubile halisi wakati huo, mwajua, mkutano halisi wa ushuhuda. Hivi hampendi kuingilia hiyo? Wakiwa tu na wakati mzuri sana, kasema, “Loo, tulia, Ndugu, utakipindua hiki chombo kabisa.”

⁹⁷ “Loo, vema nakumbuka, hilo hakika liliondolea ugumu wote, kwa kuwa mimi na Filipo tulikuwa tu tukilijadili Andiko hilo, ‘kukiwepo mtu miongoni mwetu aliyekuwa nabii,’ huku tukiwa hatuna nabii kwa muda wa miaka mia nne, na, tangu Malaki, miaka mia nne hapo kabla, nalo wazo la *nabii* lilikuwa limetoweka. Lakini wakati yule Mtu mgeni aliponiambia mahali nilipokuwa kabla hata sijaja kule, hilo lilitosha kwangu, nilijua.

⁹⁸ “Ndipo nikaangalia kote, nami nikamwona nanii, askofu wangu,” ama chochote unachoweza kumwita, “huko juu, kasisi aliyesimama pale, naye akanikunjia uso sana, kwa sababu, mwajua, nilikuwa shemasi kule. Na kwa hiyo, alinikunjia uso sana, lakini nilishawishika, nilijua Huyo alikuwa ni Yeye, kwa hiyo sikuninii. . . nikageuza mgongo wangu, na kumkimbilia, na kuanguka miguuni Pake, na kusema, ‘Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.’”

⁹⁹ Loo, ninaweza kumsikia basi akisema, “Samahani, Filipo, kamwe nisingeweza kukuruhusu uendelee, ilinibidi tu kulisimulia mwenyewe.” Mnaona? Linapokupata, unapenda kulisimulia wewe mwenyewe, ndivyo hivyo tu, kuna jambo fulani kulihusu, unapata furaha kwa kusimulia. Ni mkutano wa ushuhuda wa jinsi gani!

Naye Andrea akijaribu tu kusimama, huku Simoni akimshikilia, mwajua, akasema, “Ninafuata,” akaruka juu.

Kasema, “Ndugu, hebu nitoe ushuhuda kwa ajili yetu sote. Mnakumbuka ile siku alipotwambia ya kwamba alikuwa akishuka kwenda Yeriko?”

“Naam, ninakumbuka tukishuka kwenda Yeriko.”

¹⁰⁰ “Na jinsi ambavyo Yeye, ana haja ya kupitia Samaria? Jinsi tulivyoshangaa mioyoni mwetu, ‘Kwa nini anazunguka huko mbali Samaria, badala ya kushuka moja kwa moja kwenda Yeriko?’ Lakini Yeye alisema alikuwa na *haja* ya kupitia huko.”

Mmoja wao akasema, “Naam, hakika, ninakumbuka.”

¹⁰¹ “Mnakumbuka kule, kule chini kwenye birika la Bethesda siku ile, wakati mtu yule alipoonywa amelala pale, katika umati huo mkubwa wa watu? Naye akasema kule, ‘Amin, amin,

nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda?" Mnaona, hapana shaka ilikuwa kwamba Yeye aliongozwa aende kule, nasi tulishangaa ni kwa nini angewaendea hao Wasamaria.

¹⁰² "Ndipo tukafika Sikari, nasi... Akaketi kama kwamba amechoka, Naye akasema, 'Enendeni mjini, mkatununulie chakula.' Nasi tukaingia kisiri, nanyi mnakumbuka, na kile... jinsi sisi... kile kilichotukia. Basi tulipokuwa tukirudi tulishangaa kumwona mwanamke huyu, aliyehandikiwa sifa mbaya." Mnajua ninalomaanisha. Siku hizo, vema, iliwabidi kutiwa alama kama walikuwa—walikuwa ni wanawake wabaya.

¹⁰³ Kwa hiyo wakasema, "Tulimwona mwanamke yule, na Bwana wetu akizungumza naye. Ni jambo la ajabu jinsi gani, Mchungaji wetu akizungumza na mwanamke kama huyo! Naye huyo hapo, amesimama pale na—akiwa ametia mawimbi yake yote kichwani mwake, na—naye alikuwa na mtungi huu wa maji, na akienda kuchota maji.

¹⁰⁴ "Naye akaanza kushusha chini, vema, tukawazia, 'A-loo, yeye si wa jamii yetu, Yeye kweli atamkaripia. Basi angalieni, ametiwa alama, hebu tuone kile Yeye atakachomwambia, kwa sababu yeye si mzuri, mnaweza kuona ninii, alama yake anayovaa, kwamba amepigwa chapa. Kwa hiyo, naye hata si mfuasi wa kusanyiko letu hata kidogo, yeye hata si wa jamii ya watu wetu, kwa hiyo Yeye kweli atamkemea, angalieni tu muone.' Nasi tukaingia kisiri nyuma ya vichaka na kusikiliza kwa makini sana.

¹⁰⁵ "Nawe Simoni, nisingeweza kukufanya uinamishe kichwa chako, kwa hiyo basi, ulitaka tu kuangalia juu ya mabega ya mtu fulani. Na kwa hiyo basi tukachungulia kidogo, naye huyo mwanamke akaingiza kulabu kwenye u—ule mtungi, naye akaanza na winchi kuushusha chini, ndipo akasema, 'Nipe maji ninywe.'

¹⁰⁶ "Ndipo akageuka, alikuwa—hakuwa amemwona kamwe. Labda, alikuwa nje usiku kucha, naye alikuwa na usingizi. Na kwa hiyo kamwe hakumwona ameketi pale."

¹⁰⁷ Naye alikuwa tu ni Myahudi mwenye umri wa makamu. Alikuwa tu na umri wa miaka thelathini, lakini nafikiri kulingana na Maandiko, walisema alionekana yuna yapata miaka hamsini, kwa sababu walisema, "Unasema ya kwamba ulimwona Ibrahimu, nawe ni mtu asiyezidi umri wa miaka hamsini?" Kwa hiyo hapana shaka huduma Yake ilimchosha kidogo, mwajua. Naye akasema—Naye akasema, "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO." Hiyo ni kweli, maskini mwili huo wa duniani haukuwa na uhusiano wowote nalo. Kwa hiyo hapana shaka alionekana kama Mtu wa makamu, ameketi kuegemea ukuta pale. Naye akasema...

108 “Akasema, ‘Bwana, si kawaida, Wewe hutambui ya kwamba—ya kwamba tuna ubaguzi hapa, kwamba—kwamba Wewe ukiwa—ukiwa—ukiwa Myahudi, ungeniomba chochote, mwanamke Msamaria.’

“Mnakumbuka aliyosema? Akasema, ‘Lakini kama ungalijua ni Nani unayesema naye. . .’”

109 Sijui, usiku wa leo, kama kweli tunajua Huyu ndiye Yule aliyeshuka. Laiti tungeweza kufungua macho yetu, na kuwaona Malaika katika nafasi zao, kumwona Roho Mtakatifu (Utukufu kwa Mungu!), akiwa tayari kufanya jambo fulani!

110 “‘Laiti ungalijua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe, nami ningekupa maji usije hapa kuyateka.’ Naye akaendelea na kumwambia kuhusu kile kisima. Nanyi mnakumbuka yale mazungumzo kuhusu kuabudia Yerusalemu? Naye akamwambia ya kwamba Mungu alikuwa ni Roho, na ‘wale wamwabuduo Yeye imewapasa kumwabudu katika Roho na katika Kweli.’”

Kwa hiyo wanaona ya kwamba mazungumzo yaliendelea. “Akamwambia, ‘Nenda, kamwite mume wako mje naye hapa.’

“‘Mbona,’ akasema, ‘Sina mume yeyote.’

111 “Na, loo, Marko, hivi niliona mwonekana wa uso wako! Ulisema, ‘Huu hapa wakati mmoja ameteleza. Kuna kasoro hapa, kwa sababu kwamba anakiri Kwake, ama, kumwambia, kwamba hana mume, Naye alisema kweli alikuwa na mume. Sasa, itakuwaje?’

“Alisema, ‘Nenda, kamwite mume wako mje naye hapa,’ umoja, *mume*. Hakuwa na mmoja kama *huyo*, hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli.

“Kasema, ‘Nenda, kamwite mume wako mje naye hapa.’

“Naye—naye akasema, ‘Sina mume.’

112 “Akasema, ‘Umesema kweli. Wewe, umesema vema, kwa sababu umekuwa na watano, naye huyo unayeishi naye sasa siye wako, hapo umesema kweli.’

113 “Nanyi mnakumbuka,” kasema Andrea, “onyesho la hisia usoni mwake? Akasema, ‘Bwana,’ si kama wale makuhani walivyokuwa kule chini walipoliona likitendeka, wakasema ‘Yeye ni Beelzebuli,’ yeye alisema, ‘Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii.’” Amina. “‘Tunajua,’” sisi Wasamaria, “‘tunajua ya kwamba ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo haya, lakini u Nani Wewe?’”

114 Alikuwa—alikuwa amemtambulisha kama naniiii wake, ama—ama, alijulikana kwake kama nabii. Ilibidi awe ni nabii, Yeye hakuwahi kumwona hapo kabla. “Ulijuaje jambo hili? Bwana, naona ya kuwa Wewe u nabii.”

115 Sasa, angalieni kile. . . Mnaona, yeye alikuwa msomaji wa Maandiko, alikuwa katika Neno, labda alijua mengi juu Yake kuliko watu wengine wengi wajuavyo, hata sasa. Akasema, “Naona ya kuwa Wewe ni nabii. Nasi tunajua,” amina, “ya kwamba ajapo Masihi, ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo kama haya, haya ndiyo atakayotwambia.”

“Akasema, ‘Mimi ninayesema nawe Ndiye.’

116 “Jinsi hayo macho makubwa ya hudhurungi yalivyobadilika! Hayo mawimbi mazuri yakaanguka chini begani mwake, akauacha maskini huo mtungi wa maji, akakimbia mjini upesi alivyoweza kwenda, akisema, ‘Njoni, mwone Mtu ambaye ameniambia mambo niliyofanya. Je, hii si ndiyo ishara yenyewe ya Kimaandiko ya Masihi? Si Yeye ndiye? Je, hilo silo ambalo tumekuwa tuingojea? Hicho si ndicho kitu kile kile tunachojua kitakuja?’

117 “Pia mnakumbuka wakati tuliposhuka kwenda mjini wakati yeye. . . ?” Sasa, alikuwa kabisa, akiwa. . . Kama unajua desturi za mashariki, yeye, wanaume wasingemsikiliza, la bwana, kwa sababu alikuwa mwanamke mwenye sifa mbaya, wanaume wasingemsikiliza.

118 Lakini hebu jaribu, mtu ambaye kweli amegundua habari za Yesu, sijali walikuwa *nini*, hebu jaribuni kuwazuia kwake basi. Mtu fulani atasikiliza mahali fulani. Ukipata kushawishika kwamba ni Mwana wa Mungu, kitu fulani, mtu fulani atasikiliza. Alikuwa akiutikisa huo mji kwa ushuhuda wake. “Njoni, mwone Mtu!” Hakujali kama alipaswa kulisema au la, lilikuwa likiwaka moto nafsini mwake.

119 Alishawishika, kasema, “Yeye ameketi pale langoni. Nilitoka nikaenda kule, Naye akanielezea maisha yangu. Yamkini huyu ndiye Masihi.” Samahani, sipaswi kuwa nikipigia hicho kelele namna hiyo, kama ninyi, kizimeni. Mnaona? Kasema, “Alinielezea maisha yangu. Si Huyo ndiye Masihi?” Nao hao watu, kwa ushuhuda wa mwanamke huyo mwenye sifa mbaya, pasipo Yeye kufanya hivyo mara nyingine tena, alishawishika kabisa na ushuhuda wa yule mwanamke kwamba Huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu, kwamba Yeye alikuwa ndiye Yesu wa Nazareti.

120 Loo, huo ushuhuda, jinsi ulivyoendelea, tungeweza kuendelea katika mkutano huu wa ushuhuda. Huenda mmoja wao alisema, “Mnakumbuka siku ile ambapo yule Zakayo alipanda juu ya mti? Mnamkumbuka akishuhudia kule chini mkutanoni? Kisha kasema, ‘Nimejiandaa kwa ajili Yake, nami nitapanda juu ya mti huu,’ huko chini Yeriko. ‘Naye atakapopitia hapa, hataniona, Nitajizungushia majani yote ndani karibu nami namna *hii* na kujificha vizuri sana, nitamtazama vizuri.’

121 “Naye akaja akishuka moja kwa moja barabarani, akasimama moja kwa moja chini ya mti huo, akaangalia

juu, si kwamba tu alimwona nyuma ya yale majani, bali alijua yeye alikuwa ni nani, Akasema, ‘Zakayo,’ haleluya, “shuka chini; ninaenda nyumbani pamoja nawe kwa chakula cha kutwa leo.”

¹²² Mmoja wao huenda alisimama, huenda alikuwa ni Mathayo, na kusema, yeye yule aliyeandika hadithi hii usiku wa leo, kasema, “Ndugu, mnakumbuka, pia, wakati Yeye alipotoka Yeriko, jinsi maskini yule mzee Bartimayo kipofu, akiwa amelala pale pembeni? Nao makuhani wote, na hao wote wakasema, ‘Aisee, wewe, tunasikia unawafufua wafu, tuna makaburi yaliyojaa hao hapa juu, njoo, ukawafufue hawa. Hei, ewe nabii wa uongo, wewe *hiki, kile*, na *kinginecho*,’ wakipiga makelele. Wengine wakipiga makelele, ‘Salamu Nabii,’ na kadhalika, na wengine wakimlaani na kadhalika. Lakini alikuwa ameelekeza kichwa Chake Yerusalemu apate kwenda kutolewa dhabihu, Kalvari.

¹²³ “Ndipo maskini yule ombaomba kipofu kule chini, naye maskini mwanamke huyo Mkristo akaja, akamchukua, akasema, ‘Nini, Mama, ni kitu gani?’” Mnaona, kuna jambo *fulani* kuhusu mtu ambaye ni Mkristo, daima wako tayari kumsaidia mtu mwingine apate kumwona. “Kasema, ‘Hayo yote yanayopita ni nini?’

“Akasema, ‘Wewe ni mgeni tu? Huyu ni Yesu wa Nazareti, yule Nabii wa Galilaya. Huyu ni Mwana wa Daudi, Yule tuliyemtumainia.’

¹²⁴ “Ndipo akaanza kupaza sauti, akasema, ‘Sasa, Bwana, labda Yeye yuko mbali sana, umbali wa nusu jengo kutoka kwangu.’” Pale kwenye kuta zilizoonekana mahali alipokuwa ameketi, na mahali Yeye alipokuwa, na umbali wa zaidi ya nusu jengo la mji kutoka kwake, namna hiyo, labda moja kwa moja kwenye yadi mia moja. “Naye akaanza kulia, ‘Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu.’ Na *kwa namna fulani* akagusa upindo wa vazi Lake.

“Akasimama na kusema, ‘Mleteni hapa.’ Huyu ni Yesu wa Nazareti.”

Ni mkutano wa ushuhuda wa jinsi gani! Hivi usingetaka kuwa ulikuwa umeketi huko nje, ukiwasikiliza?

¹²⁵ Sasa, ndugu, Biblia inasema ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Yesu yeye yule. Kama ukiweka uhai wa mzabibu wowote, kama ukiweka uhai wa—wa mzabibu unaopanda kupitia kwenye matawi, na kama ukizaa tawi na kuchipusha tawi la namna *hii*, na kuzaa tunda la namna *hii*, zabibu, kama ukiwahi kutoa tawi lingine, litazaa zabibu, vivyo hivyo tu.

¹²⁶ Na Yeye ndiye Mzabibu, sisi ni matawi. Nalo tawi la kwanza lililopata kutoka kwenye Mzabibu huo, waliandika kitabu cha Matendo nyuma yake. Hiyo ni kweli. Na kama Hilo likiwahi kuzaa mzabibu mwingine, wataandika Kitabu kingine cha

Matendo nyuma yake, hiyo ni kweli, kwa sababu utazaa tunda lile lile, maana ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

¹²⁷ Kumbukeni, Yeye alifanya ishara hiyo ya nabii mbele ya nani? Myahudi na Msamaria, si Mmataifa. Kumbukeni, kuna zile jamii tatu tu, watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi; Myahudi, Mmataifa na Msamaria. Sasa, Yeye hakufanya hivyo hata wakati mmoja mbele ya Mataifa ambalo tuna kumbukumbu yake. Kwa nini? Kwa sababu Mataifa hawakuwa wakimtazamia Masihi yeyote.

¹²⁸ Hiyo ndiyo sababu siku hizi bado hawalioni, hawatazamii kitu kama hiki. Hawamwamini Roho Mtakatifu, maana hawatazamii Kitu kama hicho. Yote wanayofuatilia, ni kujiunga na kaniza, na kuandika jina lao kwenye kitabu, na kusema, “Hamna lingine.”

¹²⁹ Lakini kwa wale wanaotazamia zile nguvu, wale wanaomtazamia Roho Mtakatifu, wale wanaokutazamia kutimizwa kwa ishara za Biblia, “Sasa, itakuwa, katika siku za mwisho,” asema Mungu, “Nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili.” Sasa, wao ni . . . Naam, Yeye huwajia wale wanaomtazamia.

Sasa, kumbukeni, Yeye aliwafanyia Wayahudi ishara hiyo, wakaikataa; akawafanyia Wasamaria, wakaikubali.

¹³⁰ Sasa, kumbukeni, Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Sasa, hebu tusimame tu kwa muda kidogo na tuchukue tu muda kidogo zaidi sasa tupate hili, maana ninaamini litalishindilia kabisa, lilitie muhuri.

¹³¹ Sasa, Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu. . .” Sasa, angalieni, sikuzote kuna matabaka matatu ya watu. Mungu hukamilishwa katika tatu. Sasa, kuna mwaminio, anayejifanya mwaminio, na asiyeamini, na hilo liko katika kila kusanyiko. Unaona? Mwaminio halisi. . . Sasa, katika siku za Lutu hivyo ndivyo tu walivyokuwa wameketi, na hivyo ndivyo wanavyoketi sasa hivi, waaminio, wanaojifanya waaminio, na wasioamini.

¹³² Sasa, Ibrahimu alikuwa Kanisa teule, mwaminio aliyekuwa ametembea na Mungu. Yeye alikuwa ndiye ule Uzao, na Uzao wake ulikuwa uirithi nchi, na—naye alikuwa ndiye u—ule utaratibu mkuu wa Mungu, na wote waliokuwa pamoja naye walikuwa katika utaratibu na Mungu, watumishi wake wote wametahiriwa na kila kitu, walikuwa wakimngojea huyu mwana aliyeahidiwa. Amina. Nao walikuwa wamekuja moja kwa moja kilimani, nao hawakuwa na mambo mazuri kama Lutu, yule anayejifanya mwaminio, huko chini Sodoma. Nao Wasodoma walikuwa wasioamini.

¹³³ Anayejifanya mwaminio na mwaminio: Nao hawa hapa Malaika watatu wakija kwenye hema la Ibrahimu, Mmoja wao

alibaki na Ibrahimu, kisha wawili wakashuka kwenda Sodoma, Billy Graham wa kisasa, na kadhalika, wainjilisti mashuhuri wa siku hiyo walishuka kwenda huko, hakuna miujiza, ila tu waliwapiga kwa upofu, na kuhubiri Injili humpofusha asiyeamini. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo wakashuka, na kuihubiri Injili, na kumwita Lutu atoke. Mnaona utaratibu wa siku hiyo?

¹³⁴ Lakini kwa Kanisa teule, Ibrahimu, Kanisa halisi ambalo halikuwa Sodoma, lilikuwa limetoka Sodoma, limetoka, hawana ushirikiano na ulimwengu, Kanisa lililoitwa litoke, lililotengwa, lile Kanisa la Bwana Yesu Kristo, lililoitwa litoke, likatengwa, likimngojea mwana aliyeahidiwa. Naye Yule aliyebaki nyuma pamoja naye, alizungumza naye.

¹³⁵ Basi kumbukeni, siku chache kabla ya hapo, jina lake lilikuwa Abram, nalo jina la—la mke wake lilikuwa Sara, S-a-r-a, lakini lilikuwa limebadilishwa likawa I-b-e-r-a-h-i-m, Ibrahimu, na Sara, S-a-r-a, “binti mfalme,” *Ibrahimu*, “baba wa mataifa.” Sasa, Biblia ilisema Malaika huyu alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, Naye alikuwa tu akila mwana-kondoo, ama, vipande vya nyama ya ndama, akinywa maziwa, na kula ugali wa mahindi, Mwanadamu, mavumbi nguoni Mwake, akikaribishwa na Ibrahimu. Ndipo wakati alipokuwa ameketi pale, Yeye alisema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?” Akamwita kwa jina la—lake la kifalme, naye mke kwa jina lake la kifalme. “Yu wapi Sara, mkeo?”

¹³⁶ Alijuaje jina lake lilikuwa Ibrahimu? Alijuaje jina lake lilikuwa limebadilishwa, wote wawili? Alijuaje kwamba alikuwa—alikuwa ameo na alikuwa na mke? Kasema, “Yuko hemani nyuma Yako.” Naye Sara . . .

¹³⁷ Akasema, “Nitakuzuru.” Hilo *Mimi! Mimi*, ni kiwakilishi nafsi. Mnaona? “Nitakuzuru sawasawa na ahadi ambayo umengojea miaka ishirini na mitano kuipokea. Huyo mwana ambaye umemtazamia yuaja. Kulingana na wakati wa uhai nitakurudia.”

¹³⁸ Naye Sara sasa, wote wawili wakiwa na umri mkubwa, Ibrahimu akiwa na umri wa miaka mia moja naye Sara tisini, alikuwa huko nyuma hemani, naye akacheka kimoyomoyo, tunavyokuita, mwajua, akacheka kifichifichi, na kusema, “Hmm, mimi, mwanamke mkongwe, nipate raha na bwana wangu, naye akiwa mzee pia?” Ibrahimu. Kwa maneno mengine, kama mume na mke labda haikuwa hivyo kwao kwa miaka kumi na mitano, ishirini. Mnaona? “Ati mimi nipate raha na bwana wangu? Mimi mzee, naye ni mkongwe pia.” Wote wawili wana umri mkubwa, i—ilimshtua sana, hata kwa namna fulani akacheka kifichifichi, kama tusemavyo, akalicheka kifichifichi. “Hiyo ingewezekanaje?”

¹³⁹ Mnajua nini? Mungu angaliuchukua uhai wake papo hapo, hiyo ni kweli, kwa kutokumwamini, bali asingeweza kufanya

hivyo. Kwa nini? Alikuwa ni sehemu ya Ibrahimu, ingembidi Yeye kumchukua Ibrahimu pamoja naye. Loo, hapo ndipo neema inapoingilia, makosa yetu yote na kupotoka kwetu, Mungu hutushikilia kwa sababu sisi ni sehemu ya Kristo, neema ya Mungu ikitushikilia. “Loo, neema ya ajabu! Jinsi inavyosikika tamu.”

¹⁴⁰ Asingeweza kumchukua Sara, kwa sababu akifanya hivyo, ingembidi kumpiga Ibrahimu kwake. Hawezi kulichukua Kanisa, katika makosa Yake yote lingali ni Kanisa Lake. Vema. Hawezi kulichukua kwa sababu angemchukua Kristo, mnaona, sehemu ya Kristo, Anakuwa nyama ya nyama Yake, na mfupa wa mfupa Wake. Kuingia kwetu kwote na kutoka, na kutokuamini, na kadhalika, na machafuko, maadamu lingali kwenye Mwili huo, na heri na shari zake, neema ya Mungu ingali inalishikilia.

¹⁴¹ Naye huyo hapo. Akasema. . . Alipokuwa akicheka, Yeye alisema, “Kwa nini Sara akacheka hemani? Ni kitu gani kilimfanya Sara kucheka?” Ni telepathia ya aina gani hiyo? Nyuma Yake, huyo Malaika akimwambia Ibrahimu *hapa* nje yale Sara aliyokuwa akifanya nyuma Yake hemani.

¹⁴² Sasa, Malaika huyo alipoondoka, Ibrahimu alimwita “Mungu.” Vema. Mtu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, kasema, “Ndugu Branham, huamini ya kwamba huyo kweli alikuwa ni Mungu amesimama pale akila ndama?”

¹⁴³ Nikasema, “Hakika ninaamini. Ibrahimu alimwita ‘Elohimu.’” Kweli. Mtu yeyote anajua hiyo ni herufi kubwa B-w-a-n-a, ambalo linatafsiriwa katika Kiyunani, “Elohimu,” ambalo linamaanisha “Yeye ajitoshelezaye kwa yote.” Ilikuwa inaenda wapi, ikionyesha pale? Naye Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Ni kitu gani? Elohimu, Mungu akionekana katika mwili wa mwanadamu, Kanisa Lake, haleluya, likimwonyesha Kristo. Yesu alisema katika Yohana Mtakatifu 14:12, “Iba- . . . Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.” Hiyo ni kweli.

¹⁴⁴ Sasa, Kanisa limetoka kwenye yale matengenezo makuu ya wakati wa Kilutheri, na kisha kupitia kwenye wakati wa Wesley, na kuingia katika wakati wa Kipentekoste, na sasa linaumbika kama lile jiwe la kichwani katika ile—ile piramidi. Sasa, msifikiri ninazungumza juu ya fundisho la piramidi, bali ninaonyesha tu mfano. Na jinsi ambavyo hilo halina budi kuenea kikamilifu kabisa mle ndani kwa sababu halijatiwa saruji, limeshushwa tu mle ndani. Na jinsi ambavyo . . .

¹⁴⁵ Kuna neno tofauti lilitumiwa, kule *kuonekana* kwa Kristo, na *kuja* kwa Kristo, mnaona, maneno mawili tofauti kabisa. Mnaona? Sasa Kristo anaonekana, katika siku hizi za mwisho, katika Kanisa Lake, akilileta Kanisa Lake pamoja katika umoja, na imani, na nguvu katika Neno, vyote pamoja, ili

atakaporudi atakuta Kanisa lile lile. “Yaliyosazwa na tunutu yameliwa na madumadu; yaliyosazwa na tunutu yameliwa na nzige,” moja kwa moja hata kwa parare. Lakini Mungu alisema, “Nitarudisha, asema Mungu.”

¹⁴⁶ Urumi, na kadhalika, uliula Mti huo mzuri wa Bibi-arusi wa Kristo mpaka ukawa Kisiki. Lakini Mungu alirudisha moja kwa moja kutoka kwenye Kisiki hicho, moja kwa moja kupitia wakati wa Luther, moja kwa moja kupitia wakati wa Wesley, kupitia wakati wa Kipentekoste, na sasa liko katika Nuru ya jioni. “Nitarudisha, asema Bwana, miaka yote ambayo parare, madumadu. . . Nitalirudisha, tena, Kanisa hilo katika uzuri Wake, Kanisa hilo katika nguvu Zake.”

¹⁴⁷ Nasi tunaona ni Nuru za jioni zikija, Roho Mtakatifu akija kwa nguvu sana juu ya Kanisa Lake, mpaka ile huduma ya Yesu Kristo, katika kujulikana miongoni mwa watu Wake wote, waliketi pale wakiwa na imani ya kumshusha chini, nguvu na karama zikifanya kazi miongoni mwao, kunena kwa lugha, kufasiriwa kwa lugha, na ishara, na maajabu, na miujiza. Ni kitu gani? Kristo miongoni mwa Kanisa Lake, akijitayarisha kumchukua.

¹⁴⁸ Katika kufunga, huenda nikasema hivi: Huko nje baharini usiku huo, kumalizia ushuhuda wao, tutaanza kuwaombea wagonjwa basi, huko nje baharini usiku huo, wakati walipokuwa na mkutano huu wa ushuhuda, walikuwa na wakati mzuri sana, lakini wakakosea, katika msisimko wao wote wa ule uamsho wao mkuu ndio kwanza wawe nao, waliondoka bila Yeye.

¹⁴⁹ Sasa, nashangaa tu, ndugu, kwa nia njema kabisa, kama hilo silo tu karibu kama lile lililotendeka katika siku hizi za mwisho. Tuna majengo mapya, tu—tumejenga vitu vipya, tumeongeza mashirika yetu, tumefanya mengine yote, na kuweka mabilioni na mabilioni ya dola hapa nje, huku tukisema ya kwamba Kristo yuaja mara moja. Mbona, watu ni werevu sana kujua. . . wanajua bora kuliko hivyo. Maneno ye—yetu hunena. . . maneno yetu hunena kwa sauti kubwa kuliko. . . Matendo yetu hunena kwa sauti kubwa kuliko maneno yetu, hasa. Hiyo ni kweli. Sisi ni ninii tu, inaonekana, tunapigana na hewa.

¹⁵⁰ Nao hao hapo, wakaondoka, na wote walikuwa wamesisimkwa sana kuhusu huo mkutano, hata wakasahau kuambatana na Yeye, ndipo shida ikaingia. Hapana shaka ibilisi aliinuka nyuma yao, akasema, “A-haa! Hao hapo katika mpangilio wao mkubwa. Kwa hiyo huu ndio wakati wangu wa kuingia.” Huyu hapa akaja, akashuka moja kwa moja, akaanza kuwapulizia maskini pumzi yake ya sumu, “Siku za miujiza zimepita. Yote imekuwa ni lundo la mihemuko na msisimko.”

¹⁵¹ Mawimbi yakaanza kuja, huku ibilisi ameketi kwenye kila wimbi, akisema, “Tutampata. Tutaizamisha.” Ndipo maskini mashua hiyo ikajaa maji, makasia yakavunjika, na

nguzo ya mlingoti ikaanguka chini, matumaini yote yalikuwa yamekwisha, maskini mashua hiyo ndogo ikiinuka, imejaa maji, nayo ikalowa maji.

¹⁵² Na sasa, matumaini yote yamekwisha, na, lakini mnajua nini? Nina furaha sana kuwaambia jambo hili sasa: Walipomwacha, Yeye alifanya nini? Alipanda kilima kirefu kuliko vyote n—nchini. Kadiri alivyozidi kupanda juu, ndivyo alivyoweza kuona mbali zaidi, Naye alikuwa akiwaangalia wakati wote. Ninaamini amefanya jambo lilo hilo, sivyo? Akatuona katika machafuko yetu. Naam. Hao hapo katika machafuko mabaya sana, ndipo baada ya kitambo kidogo, kwenye dhoruba, ndipo matumaini yote yakaisha kwa ajili ya uamsho mwingine kote katika nchi nyingine, walikuwa wanaenda kuzamishwa kabla hawajafika kule, Huyu hapa akaja akienda kwa miguu juu ya bahari, akiwaendea moja kwa moja, na ninii hasa . . .baada ya mkutano huo wote wa ushuhuda, wangali walimwogopa, wakasema, “Inaonekana ni mzuka.” Naam. Naam. “Hue- . . .Huenda akawa ni kivuli.”

¹⁵³ Alipotuacha, alipanda akapita Kalvari, akaenda juu zaidi, akapanda kupita, akapanda mpaka akapita jua, mwezi, na nyota, kama vile kanisa la Ndugu Outlaw lilivyokuwa likiimba hivi majuzi usiku, kasema, “kupita Jupita, Zuhura, Neptuni, na Mirihi.” Alipanda mpaka akafikia ile Njia ya Kilimia Cheupe, kisha akaingia Mbinguni, juu ya Mbingu, naye ameenda moja kwa moja akapita Mbingu, na kupata Jina lililo juu ya kila kitu kinachotajwa Mle ndani; inambidi kuangalia chini apate kuona Mbingu. “Nalo jicho Lake liko kwenye shorewanda,” nami ninajua Yeye anaangalia usiku wa leo, sivyo? Hiyo ni kweli.

¹⁵⁴ Basi akawajia akitembea juu ya maji, Kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia, nao walikiogopa. Hilo si ni la ajabu? Kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia, walikiogopa. Na ndivyo imekuwa sasa, Kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia watu kutoka kwenye ukomunisti, kutoka kwenye mambo haya yote, Wamarekani wanakiogopa, wanasema, “Kinaonekana ni mizuka. Huenda ikawa ni *hiki* ama *kile*.” Msifanye hivyo.

¹⁵⁵ Kwa nini usimwalike aingie chomboni usiku wa leo, useme, “Njoo, Bwana Yesu.” Ndipo kitu hicho kitatulia, haitachukua muda mrefu kabla hatujafika ufukoni. Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu sasa.

¹⁵⁶ Baba yetu wa Mbinguni, njia fidhuli sana ya kulazimika kuleta ujumbe kwa kundi la watu wenye akili, lakini nina hakika, Baba, ya kwamba Wewe utawafasiria katika—katika—katika mtazamo uliokusudiwa, kwamba litaenda katika maana ya upendo na ushirika, na—na kwa ajili ya imani kwa watu.

¹⁵⁷ Na sasa, Baba, tunaomba ya kwamba utusamehe makosa na mabaya yetu yote, tunaomba ya kwamba Roho Wako Mtakatifu atakuja juu yetu sasa. Tumesema ya kwamba Wewe ni yeye yule

jana, leo, na hata milele, basi kazi ulizofanya Wewe, Kanisa lingezifanya pia.

158 Pia tulinukuu Maneno Yako, Bwana, Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Lako halitapita, Nawe ulisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Sasa, wakati wa Mataifa umewadia, Wewe siye Mungu ambaye angelisha sehemu ya watoto Wako chakula kimoja kizuri, na kukiacha mezani kwa ajili ya wengine, kwa sababu Wewe ni mwenye haki, mwenye heshima, mtakatifu, huna upendeleo.

159 Na ulipowapa Wayahudi ishara yao ya mwisho, wengi wao walitambua ya kwamba hilo ndilo lililonenwa, Maandiko yalisema hilo lingetimia, na hilo hapo. Wakati ulipoliendea kundi hilo dogo la Wasamaria, waliotupwa nje, waliliamini, jambo la kwanza lilipotukia, waliliamini. Na sasa, Wewe huyu hapa mlangoni pa Mataifa, huo ulikuwa ndio mwisho wa wakati wao, na huku ni kumaliza kwa wakati wa Mataifa. Mungu, tunaomba ya kwamba watu hawa wote humu ndani usiku wa leo, walio na karama ya Roho Mtakatifu, wataachilia imani yao kwa Mungu, na kwamba Mungu apate kuutumia kuuleta Uwepo wa Yesu Kristo miongoni mwetu, usiku wa leo. Tunaomba hayo, katika Jina Lake, na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

160 Mimi, sijui, nadhani ilitupasa kufungia hapa mapema sana, lakini tuliniini tu. . . Kesho usiku ha—hatutachelewa hivi. Tutachukua tu muda kidogo na kufanyiza m—m—mstari wa maombi kadiri tuwezavyo kuupanga, na kuwaweka kwenye huo mstari na kuwaleta huku juu nasi tutawaomba wagonjwa.

161 Sasa, Billy yuko wapi? Moja, moja hadi mia moja? Alisema alisambaza kutoka moja hadi mia moja, kadi za maombi. Vema. Sasa, hebu tuwapange sawasawa wanavyokuja sasa. Namba moja, ni nani aliye na kadi hiyo ya maombi? Ni herufi gani? Sisi. . . Nini? I, I, kama “Indiana,” I.

162 Vema, I, moja. Ni nani aliye na hiyo kadi ya maombi? Huyu mama? Njoo papa hapa, Mama, tafadhali. Namba mbili, kama utainua tu mkonu wako sasa, namba mbili. Kama. . . Nisaidieni, baadhi. . . Loo, mbili? Asante. Namba tatu. Ni nani aliye na namba tatu? Vema, Bwana. Nne. Vema. Sasa, hiyo ni kweli enyi mabawabu. Tano, tano. Nisaidie, mtu fulani, tafadhali. Kadi ya maombi tano, sita, sawa. Vema, sita, saba, nane.

163 Nani aliye na namba nane? Sikuiona. Ni huyu mama hapa? Ninaamini ndiye. Hiyo ndiyo. Vema, nane, tisa, namba tisa. Huyu mama hapo? Namba kumi. Vema, Bwana. Kumi na moja.

164 Ninafanya hivi kuwazuia wasikanyagane, mwajua, na, hii ni nyumba ya Mungu, sio uwanja wa michezo. Mnaona? Kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na nne. Siioni. Kumi na nne? Vema. Kumi na tano, kumi na sita, kumi na sita, kumi na saba, kumi na saba.

165 Labda mtu fulani ni kiziwi, sasa, ama mtu fulani hawezi kusimama kutoka kwenye kiti, ama kitu fulani, tutaenda... Nasi tutamwombea kila mtu anayekuja na anataka kuombewa. Baadaye kidogo, sisi, huu ni mkutano mdogo tu wa utangulizi usiku wa leo, tutachukua muda mwingi kidogo tunapoendelea.

166 Ni wapi hapo? Yapata kumi na tano, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa, ishirini, ishirini, ishirini, ishirini, ishirini. Vema, vema, hebu... huenda ikawa ni mtu fulani ange-... Vema, mtu fulani ameingia tu na kutoka. Billy alisema kwamba hawawezi kusikia vizuri sana huko nyuma.

167 Vema. Ningetaka kuuliza hili basi. Hebu tungoje kwa dakika moja sasa. Ninataka ishirini, iwapo walitoka nje, waweke moja kwa moja mstarini, tutaanza moja kwa moja. Vema. Sasa, ni wangapi hapa ndani wasio na kadi ya maombi, nawe unaamini ya kwamba—ya kwamba una imani ya kutosha kuamini Mungu atakuponya? Hebu tuone mikono yenu, kila mahali sasa, hivyo ndivyo ilivyo. Vema. Yote yamekwisha tu.

168 Sasa, wakati mabawabu wanaposhughulika kule chini, ningetaka kuwaulizeni jambo hili, niwape Andiko. Kama ukiwahi wakati mmoja kunishika nimetoka nje ya Biblia hii, njoo, uniambie. Unaona?

169 Vema. Angalia, kulikuwa na mwanamke wakati mmoja ambaye hakuwa na kadi ya maombi, tungesema, namna hiyo. Inasikika... hiyo ni ninii yangu... natumaini halisikiki la kukufuru. Lakini alikuwa anatokwa na damu, naye akasema, “Kama nikiweza tu kugusa vazi Lake, nitakuwa mzima.” Mnakumbuka hadithi hiyo? Hakika, mnakumbuka. Vema.

170 Ndipo a—akaligusa vazi Lake. Sasa, nje... Asingeweza kuhisi jambo hilo kikawaida, kihalisi, maana vazi la Kipalestina linapwaya, ni joho, na chini ya hilo kuna vazi la ndani, kuzuia mavumbi miguuni mwao, wala Yeye kamwe asingeliligusa. Aligusa tu upindo wa vazi Lake.

171 Na hata mtume Petro alimkemea, ama, alimkemea aliposema, “Ni nani aliyenigusa?” Akasema, “Lakini naona kwamba nimekuwa dhaifu. Nguvu zimenitoka.”

172 Sasa, ni wangapi wenu wanaoamini ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele? Sasa, angalia kundi hili tukufu la wachungaji *hapa* sasa. Sasa, ndugu, hivi Maandiko hayatufundishi ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu, sasa hivi, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Sasa, mnaona?

173 Ni wangapi huko nje wanaoamini Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na...? Sasa, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, Yeye angetenda vile vile kama alivyotenda wakati huo. Hiyo ni kweli? Sasa, ungejuaje Yeye alikuwa akitenda? Sasa, jambo ndilo hili. Ndio kwanza nimalize kusema Mungu yuko ndani ya watu Wake. Yote aliyokuwa Mungu, aliyamimina ndani ya Yesu. Mnaamini hilo? Yeye alikuwa ndiye Utimilifu wa Uungu

kwa jinsi ya mwili. Na yote aliyokuwa Yesu, aliyamimina ndani ya Kanisa, Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli? Kwa hiyo ni Mungu ndani yetu, Mungu ndani yako.

¹⁷⁴ Si... Haikufanyi chochote, si “mlima mtakatifu,” ama “kanisa takatifu,” ni—ni Roho Mtakatifu; si watu watakatifu, Roho Mtakatifu. Mnaona? Ni Roho Mtakatifu *ndani* ya watu; si watu watakatifu, Roho Mtakatifu. Mnaona? Na jambo ndilo hilo.

¹⁷⁵ Na katika Roho huyu Mtakatifu, ana karama. Nazo karama za ofisi za Kanisa ni mitume, manabii, walimu, wainjilisti, wachungaji. Hiyo ni kweli? Yote ni kwa ajili ya kulijenga, ama kuliweka Kanisa pamoja, kuliweka katika utaratibu (Hivi wao...? Niambieni wakati mkiwa tayari. Sawa.), kuliweka katika utaratibu.

¹⁷⁶ Sasa, nitawaomba mnifanyie jambo moja sasa, tafadhali. Kama ukitupa tu... Wasikilizaji wengine, natumaini mnaweza kunielewa vizuri sana sasa, msisogeosogee sasa, mnaona, kaeni tu kimya kabisa. Tangu wakati huu na kuendelea msisogee, mnaona, maana ni chini ya upambanuzi. Na unaposogea, wewe ni roho, nawe ni, unatambua ya kwamba wewe ni roho, kama siyoye, umekufa. Unaona? Na mradi tu wewe ni roho, na upako wa Roho hapa... .

¹⁷⁷ Huyu Roho Mtakatifu ana mawasiliano na kila roho humu ndani. Ni wangapi wanaojua hilo? “Roho za nabii hutii...” Mnaona? Kwa hiyo anawasiliana. Ndipo unaposogea, unaona, hilo linakatiza. Unaona? Sasa, kutakuwako na *hawa* jukwaani wakisogea, kwa sababu nimewasiliana na mtu huyo. Mnaona? Halafu wanakuja, na mara Roho Mtakatifu anapozungumza nao, basi mnaona, halafu wengine wanaosimama, kitu fulani kitasogea na kitasogea, *hivi*. Hakukuwako na hata mmoja ambaye... Unaona, hujui tu la kufanya, ndipo umechanganyikiwa tu. Kwa hiyo mkipenda, kwa yapata dakika kumi tu kupitia mstari huo, ama kumi na mitano.

¹⁷⁸ Sasa, kabla sijafanya jambo hili, nitawaulizeni jambo fulani. Ni wangapi katika mstari huu ambao hatufahamiani? Inua mkono wako. Kila mmoja wenu ni mgeni. Ni wangapi katika kusanyiko ambao ni wageni kwangu? Inueni mikono yenu, kama unajua ya kwamba sijui lolote kukuhusu, inua tu mkono wako. Mnaona?

¹⁷⁹ Nadhani kila mtu hapa, kadiri niwezavyo kuona, kwamba simjui mtu yeyote. Sijui ila yapata wawili wa wahudumu hawa hapa jukwaani, wawili au watatu wa hawa, Ndugu Kopp na hao wengine, ninawajua, lakini huko nje kwenye kusanyiko, sioni mtu mmoja huko nje ambaye ninaweza kumtambua nipate kulitaja jina lake wakati huu.

¹⁸⁰ Lakini kila mmoja wenu, Mungu anawajua, Yeye anajua papo hapo mnapoketi. Kwa njia yangu ya kumwona Mungu, Yeye alijua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu ya kwamba

ungekuwa umeketi pale, kama Yeye hana kikomo. Hakika, Yeye hana kikomo, alijua kila kitu. Hiyo ndiyo sababu Yeye angeweza kujua mwisho tangu mwanzo, Yeye hana kikomo.

¹⁸¹ Sasa, sasa, hapa, huyu ndiye, mgonjwa huyu hapa? Waweza kujongea tu karibu kidogo, Mama? Sasa, hii hapa mandhari halisi ya Biblia ya Yohana Mtakatifu mlango wa 4, yale tu niliyomalizia kuyazungumzia, mmojawapo wa mifano ya huo mkutano wa ushuhuda. Huyu hapa mwanamume mzungu, mwanamke mweusi, huyo alikuwa ni Yesu, Myahudi, na mwanamke Msamaria, jamii mbili hasa. Na kwa hiyo, alijaribu kumwambia jambo hilo, kwamba hilo halikuwa jambo la kawaida, bali Yeye alimwambia, kwanza, ya kwamba . . . lakini alimjulisha ya kwamba Mungu aliwaumba watu wote.

¹⁸² Kila mtu ni, sisi sote tumetokana na Adamu na Hawa, hao ndio baba na mama yetu sote, wanadamu wote. Mahali sisi, tulipolelewa, rangi ilitubadilisha, weupe, kahawia, weusi, wa manjano wowote wale, haina uhusiano wowote, kila mmoja wetu angeweza kumpa mwenzake damu, sisi sote, Mungu aliwaumba wa mataifa yote, damu moja. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo maskini kitu hicho kilikuwa kimekufa wakati Yesu alipokuja, ubishi huo wa kale waliokuwa nao, aliwajulisha ya kwamba Mungu alikuwa ni Mungu wa Wasamaria, sawasawa tu na alivyokuwa wa Myahudi, naye Baba alikuwa akiwatafuta watu kama hao ambao wangemwabudu katika Roho na Kweli, haidhuru walikuwa nini.

¹⁸³ Petro alisema, kule juu, alisema, ile nyumba, “Naona ya kuwa Mungu, hana upendeleo wa taifa lolote, bali wote wamchao.” Hiyo ni kweli. Akitoa wito kwa . . .

¹⁸⁴ Vema, hii hapa Yohana Mtakatifu 4 hasa. Hatufahamiani. Sasa, hili linapaswa kulitatua. Hebu niwaambie, mimi ni ndugu yenu, mimi ni Ndugu Branham, ndugu yenu. Lakini, mimi si mhubiri, ambalo mnajua, ni—ningependa kuwa, bali si—sina elimu ya kutosha kuwa nikijiita mhubiri. Lakini, hii ndiyo huduma yangu aliyonipa, karama. Na karama hiyo ni kulitikisa Kanisa lipate kukutambua kule Kuja kwa Kristo, kurudi kwa Roho wa Mungu Kanisani.

¹⁸⁵ Yuko juu yenu, Roho yeye yule, huenda isiwe karama ile ile, bali Roho yeye yule, kuna madhihirisho mbalimbali, bali ni Roho yeye yule wakati wote. Roho Mtakatifu yeye yule uliye naye ndiye Roho Mtakatifu yeye yule niliye naye, Roho Mtakatifu yeye yule tuliye naye, sote tu watoto wa Mungu.

¹⁸⁶ Halafu basi, sababu ya sisi kuja pamoja, kiroho sasa, basi huyo Roho Mtakatifu yupo. Na kama magonjwa ni . . . Ndipo watoto wakija mahali Roho huyo alipo, Yeye—Yeye anawatambua, na anaweza kukutambua. Ni ninii, kama ninii . . . karama ya unabii, ama, si karama ya unabii, sijui, niseme tu ni Kristo, mnaona, akishuka miongoni mwetu, kwa sababu ukianza kubandika namna fulani ya jina kwenye kitu fulani,

umevurugika kabisa, kwa hiyo hebu tuseme tu Bwana wetu Yesu Kristo yuko katikati yetu. Mnaona? Hebu tuseme tu hivyo.

¹⁸⁷ Sasa, tumesimama hapa tukizungumza na mwanamke huyu. Simjui, sijawahi kumwona, anaonekana mwenye afya tele, huenda—huenda akawa na matatizo ya kinyumbani, matatizo ya kifedha, huenda akawa ni mwigaji, mimi. . . huenda akawa ni Mkristo, huenda akawa ni mwenye dhambi. Simjui, alikuja tu hapo. Lakini lolote Yeye atakalomwambia, yeye atajua kama ni kweli ama si kweli, atakuwa tayari kukubali hilo. Vema, kama anaweza kumwambia kile kilichokuwa, kama alivyomwambia Filipo, kama alivyomwambia Nathanaeli, kama alivyomwambia yule mwanamke kisimani, ama, kama Yeye akimwambia yaliyokuwako, hakika anaweza kuamini kwa ajili ya wakati ujao basi. Hiyo ni kweli? Nyote mtaamini, kama atafanya hivyo?

¹⁸⁸ Sasa, sisi hapa, *Hii* hapa Biblia, *huyu* hapa mwanamke, na sisi hapa tumesimama papa hapa mbele zenu nyote huku tumeinua mikono yetu, kwamba hatujawahi kukutana hapo awali, hatufahamiani. Nasi ni wa jamii tofauti ya watu, yeye ni. . . Mimi ni Mwanglo-Sakson, naye ni Mwafrika. Sasa, sisi hapa, kikamilifu tu iwezavyo kuwa.

¹⁸⁹ Sasa, Dada, ili tu kuwasiliana nawe, sababu ya mimi kukuita *Dada*, kwa sababu nilipoangalia kote, Roho alinishika, nami nilijua ulikuwa Mkristo. Hiyo ni kweli, wewe ni Mkristo. Sasa, sikujui. Sasa, ninasimama tu hapa, unajua ninafanya jambo fulani, ninawasiliana tu na roho yako, nikiianzisha kutoka karibu na watu hawa wengine, nikikuvuta tu kama mtu mmoja.

¹⁹⁰ Sasa, kama Kristo anaweza kunitumia, kama karama, sasa, huenda akaweka upako Wake juu yangu, hana budi kuuweka juu yako wakati uo huo, la sivyo hautafanya kazi, inahitaji sisi sote wawili kuufanya utende kazi. Yule mwanamke aligusa vazi Lake, Yesu hakujua ni nani aliyefanya hivyo, bali Yeye alisema, “Naona kwamba nguvu zimenitoka.” Mnaona, haikuwa Yeye, akasema, “Imani yako imekuokoa.” Unaona? Ilikuwa ni imani yake.

¹⁹¹ Sasa, sikujui, lakini kama Yeye atakwambia jambo fulani kuhusu maisha yako, labda kitu fulani kilichokuleta hapa, mtu fulani uliyemsimamia, jambo fulani ambalo umefanya ambalo ni baya, ama chochote kama hicho, utajua kama ni kweli ama si kweli, na ndipo utaamini. Bwana Mungu na alijalie, ndilo ombi langu.

¹⁹² Sasa, mnaona linaniweka mahali gani? Huu hapa wakati sasa ambapo yale niliyohubiri na kuwaambia kumhusu Yeye, hayana budi kutenda, la sivyo, au nilisema uongo, Biblia ilisema uongo, Kristo hayuko hai, ama mnaona, ni ama dini yetu ni ya kweli au si ya kweli. Haina budi kuonyeshwa sasa hivi miongoni mwa kundi hili zuri la watu hapa. Mnaona? Hawa hapa wahudumu wa Kristo wameketi hapa.

193 Sisi...Nimesimama mbele ya mamia ya maelfu, hata nisingeweza kuzungumza lugha yao, na kuona jambo hilo likitukia tu, mbele ya makafiri, wachawi, na wale wanaowaita “watu watakatifu” wa India, na watembea motoni, na kadhalika na kuona nguvu za Mungu zikishuka na...Lakini Yeye ni Kristo, kama sivyo, ninataka kujua mahali alipo, ninataka kumwona.

194 Naam. Huyu mwanamke, si *mnafikiki*, amesimama hapa kwa ajili ya jambo fulani, na jambo hilo, ambalo halina budi, yeye kweli, kulingana na daktari, anapaswa kukabili upasuaji. Hiyo ni kweli. Na upasuaji huo ni uvimbe. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa, unaamini ya kwamba Yeye anajua huo uvimbe ulipo? Unaamini Yeye angeweza kuniambia? Unaniamini mimi? Uko kwenye titi, uko kwenye titi lako la kushoto. Hiyo ni kweli. Vema. Nenda, amini sasa, na haitakubidi kufanyiwa upasuaji. Kama utaamini kwa moyo wako wote, Mungu aliye Mbinguni atakuondolea huo.

195 U hali gani, ewe msichana? Hatufahamiani, nadhani. Ni mwanamume na mwanamke tu wamekutana, lakini Yesu Kristo anatujua sote wawili, Yeye anajua yote kukuhusu, Yeye anajua yote kunihusu mimi; mimi ni mtumishi Wake tu. Nawe unaamini ya kwamba Yeye yupo hapa na angeweza kunifunulia jambo fulani kukuhusu wewe? Ingekufanya uwe na imani Kwake kujua ya kwamba Yeye—Yeye yupo hapa? Je, utakubali kile unachoomba? Je, . . .? Ungefanya hivyo.

196 Mtu huyo aliyeketi pale ameinua mkono wake kwenye kidevu chake, namna *hii* akiketi papa hapa, ameketi pale akiombea ugonjwa wa wasiwasi, amini tu kwa moyo wako wote, wasiwasi umekuondokea sasa. Sasa, hiyo ni kweli? Inua mkono wako.

197 Ninataka kuwaulizeni aligusa nini. Alikuwa na imani ya kumleta Roho Mtakatifu kutoka *hapa* na kumpeleka kwa mtu huyu. Sijawahi kumwona maishani mwangu, yeye ni mgeni kwangu, nijuavyo mimi, bali alikuwa na imani. Hiyo ndiyo inayohitajika, imani ya kufanya jambo hilo. Amini tu.

198 Mimi huangalia tu Nuru. U—umewahi kuona picha Yake? Ninaamini wanayo hapa, ama watakuwa nayo. Imepitia upande huu kutoka kwako ikatoka nje, ninaiona imesimama juu ya yule mtu pale, ilibidi tu niliseme. Sasa, yule pale mtu ameketi pale, mtu tu aliyeketi mkutanoni . . .? . . .

199 Nawe ni mgonjwa, umekuwa kwa daktari, umepata ushauri kutoka kwake, bali unaogopa ushauri wake. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Hakuna kitu kiovu, ni sawa, ni tatizo la wanawake, hiyo ndiyo shida uliyo nayo. Ninaweza kumwona wakati wa uchunguzi, yale aliyosema. Ni sawa kwangu kusema ni kitu gani? Unataka nikwambie ni nini?

200 Kwa kweli ni, mahali fulani, ni mbegu iliwekwa mahali si pake, chembe hai, nayo imenaswa kwenye ile tyubu, badala

ya kushuka na kuingia kwenye ovari. Inaitwa “tyubu iliyotiwa mimba,” naye anataka kufanya upasuaji, nawe unaogopa huo upasuaji. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Hiyo ni kweli. Beatrice, unataka kuponywa? Nenda, ukamwamini Bwana Yesu Kristo nawe utaponywa.

Unamwamini Bwana Yesu, kwamba yale ninii, yote yaliyotabiriwa na Biblia yatatimia?

²⁰¹ Mwanamume, hatufahamiani. Unaamini Bwana Yesu yuko hapa kukusaidia? Unaamini kama Yeye atanifunulia kile unachotaka Kwake, kwamba utapewa? Unaamini.

²⁰² Naendelea kumwona mwanamke akija. Aliyeketi papa hapa chini akiniangalia, anaugua moyo...shinikizo kuu la damu huku amevaa miwani, huzichana nywele zake nyuma, ambazo...

Hivi hamwoni Nuru ile ikining’inia juu ya yule mwanamke pale? Angalia. Inua mkono wako, Mama. Haya basi.

Unaamini kwa moyo wako wote sasa? Basi nenda nyumbani ukapone.

Simjui huyu mama, sijawahi kumwona maishani mwangu, ni mgeni kwangu.

²⁰³ Hiyo ndiyo shida yako. Umekuwa na imani ya kutosha kugusa vazi Lake kugeuka namna hiyo, vema, usingeweza kukosa kuliadini hilo, sivyo? Utapata uponyaji wako basi.

²⁰⁴ Ninataka kuwaulizeni, angeweza kugusa nini huko nje? Yuko, nadhani, futi thelathini kutoka kwangu. Yeye hakunigusa, hanigusi mimi, yeye anamgusa Yeye. Mnaona? Hivyo ndivyo ilivyo. Alimgusa Yeye, Naye akajibu tu, mnaona. Laiti Kanisa lingeamka kwa jambo hilo na kutambua hilo ni nini! Hmm!

²⁰⁵ Vema. Iweni na kicho sasa. Msiogope. “Msiogope; Ni mimi,” Yeye alisema. Ni Bwana Yesu, mnajua si mimi, maana...Na haina budi kuwa ni Roho fulani na nguvu, kwa hiyo chochote unachowazia ndivyo ilivyo; kwangu mimi ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, akithibitisha yale hasa aliyosema.

²⁰⁶ Sasa, Bwana, bila kukujua wewe nasi tukiwa hatufahamiani, kama Bwana Yesu atafunua jambo fulani kukuhusu, ama jambo fulani unalotaka, ama jambo fulani unalotaka kwa ajili ya mwingine, ama lolote lile, utamwamini Yeye, sivyo?

²⁰⁷ Uko tayari kufanyiwa upasuaji, unapaswa kufanyiwa upasuaji mwingine, maana umefanyiwa mmoja, na upasuaji huo ulikuwa wa figo, vijiwe, nawe umerudi tena. Hiyo ni—ni hali ya kemikali ya mwili wako inayosababisha hayo, na hicho ndicho kitu pekee kinachoweza kusababisha...kuwepo kamwe ni kwamba Mungu aondoe sehemu ya kemikali ya mwili wako ambayo—ambayo inaufanya upasuke, angalau hivyo ndivyo huyo mtaalamu alivyosema.

208 Ha! Mke wako amesimama moja kwa moja kule chini kwenye mstari wa maombi, kwa ajili ya, akitaka, ugonjwa wa figo pia. Vipi kuhusu wewe ugeuke tu, ushuke uende kule, uweke mikono yako juu ya mke wako na kumwombea? Je, unaamini kwa moyo wako wote Bwana Yesu ata—atafanya, na kutekeleza, na kutujalia, na kumpa—kumpa afya?

209 Baba yetu wa Mbinguni, wanapowekeana mikono, ninamhukumu ibilisi aliyefanya hivyo, na jalia wote wawili waponywe, na waende nyumbani wakapate afya kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Tujalie, Baba. Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba. Amina.

210 Vema, usiwe na shaka moyoni mwako sasa, amini kwa moyo wako wote. Ondoka mstarini, Dada, nenda moja kwa moja pamoja naye, nenda nyumbani, na usahau kuhusu kuwa nao kamwe, na upone.

211 Ninaamini Bwana Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ninaamini ya kwamba Yeye yupo hapa sasa. Ninaamini Yeye ni Ua la Uwandani, Nyinyoro la Bondeni, Nyota ya Asubuhi. Ninaamini ya kwamba Yeye yupo hapa leo, akitokea miongoni mwa watu, akiwaonyesha ya kwamba mwisho umekaribia, na kwamba hivi karibuni Yeye yuaja kulinyakua Kanisa, na huduma ya wahudumu Wake inaumbika moja kwa moja ikawa huduma Yake Mwenyewe aliyokuwa nayo hapa duniani, kulinyakua Kanisa zima, ninaamini hilo kwa moyo wangu wote.

212 Vema. Sasa, tafadhali... Vipi...? Mimi ni... Nimepitisha wakati wangu, samahani. Hebu tuwe na mwanamke huyu mmoja hapa. Basi, waweza...? Hebu—hebu kidogo.

213 U hali gani, Dada? Ulikuwa hapa juu, kwa hiyo nafikiri unahitaji kuombewa, ama, nitawaombea hao wengine, lakini ninamaanisha wewe kwa ajili ya upambanuzi, ama, kile tungekiita, mnaona, chochote kile.

214 Unaniamini mimi kwamba ni mtumishi Wake kwa moyo wako wote? Shida yako iko kifuani mwako. Hiyo ni kweli. Lakini kunaendelea kuwa na mtu mwingine anayetokea hapo. Ni mume wako, hayuko hapa, bali ulikuwa naye akilini mwako, ulikuwa ukimwombea, hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yake ni nini? Iko mgongoni mwake. Kwa hiyo, hiyo ni kweli, sivyo? Sasa, unaamini utaenda nyumbani, umkute mzima? Vema. Basi endelea tu moja kwa moja kwenye hilo...?.. Kama uta—utaamini kwa moyo wako wote, nawe utalipata jinsi tu unavyoamini. Sasa, kama huna shaka, utalipata hivyo tu.

Unaamini kwa moyo wako wote?

Dada, unaamini Mungu anaweza kuponya yabisi kavu na kumponya mtu? Zidi tu kusonga mbele, ukisema, “Mungu asifiwe, kwa kuniponya.”...?...

215 Sasa, unaamini jambo lile lile, kwamba wasiwasi na yabisi kavu vitaondoka, nawe utakuwa mzima? Basi endelea moja kwa moja ukisema, “Asante Bwana.” Amini, amini ya kwamba Yeye huponya.

216 Angalia huku unapokuja, Dada. Wewe. . . Mungu anaweza kuponya ugonjwa wa moyo kama vile anavyoweza kuponya kitu kingine chochote. Hivi huamini hilo? Unaamini kwa moyo wako wote? Basi inua mikono yako, useme, “Ninaukubali.” Nenda zako moja kwa moja ukimpokea Kristo, na uwe mzima, katika Jina la Bwana Yesu. Nenda ukiamini.

217 Vema. Mtu huyu amelemazwa kwa kujikwaa. Njoo huku, Bwana. Ninaona umelemaa. Niangalie na uamini. Utaamini? Vema. Kama utaamini, yabisi kavu yote itakuacha, nawe utaenda nyumbani, uwe mzima. Unaamini Yeye atafanya hivyo? Basi kama unaamini, endelea tu kutembea na kusema, “Mungu asifiwe.” Ninataka kukuwekea mikono unapopita. Pitia hapa na kusema, “Asante,” useme, “Shukrani na sifa ziwe kwa Mungu,” na uamini kwa moyo wako wote kwamba ni. . . ? . . .

218 Ninataka kukuuliza jambo fulani. Pamoja na Kitabu hicho cha thamani chini ya mkono wako, vipi kama ningeweka tu mikono yangu juu yako? Ungeamini ungepona? Basi, katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukapone. Amina.

219 Vema. Njoo. Unawazia nini, Dada? Maskini vipindi hivyo vya wasiwasi vimekuwa vikikusumbua. Unaamini vitaondoka sasa? Unapopita chini ya kivuli cha msalaba, endelea kushangilia, ukisema, “Havitanisumbua tena.”

220 Angalia huku, Bwana. Una mambo mengi yanayokusumbua, kama tezi kibofu na kadhalika, bali jambo lako kuu ni ugonjwa wa moyo. Nenda zako na useme, “Nimeponywa katika Jina la Bwana Yesu.” . . . ? . . . moyo wako wote. Amini tu kwa moyo wako wote.

221 Angalia huku, Mama. Unaamini ugonjwa wako wa mgongo utapona, kisha uende nyumbani na kuwa mzima? Vema. Endelea tu kutembea, ukisema, “Mungu na ashukuriwe, Yeye atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo.”

222 Mama huyo ana shida ya wanawake, na pia ninaona anasumbuka, anasongwa moyoni mwake. Njoo upite moja kwa moja na kusema, “Ninaamini kwa moyo wangu wote. Ninaenda nyumbani, utaacha kunisumbua, nami nitakuwa mzima.” Amini sasa, useme, “Ashukuriwe Mungu, Yule atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo.”

223 Huyu hapa mtu anakuja, inaonekana kana kwamba anapaswa kuwa na imani. Vipii kama ukipita tu hapa, nikuwekee mikono? Biblia inasema “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono juu ya wagonjwa watapata afya.” Unaamini hilo? Njoo moja kwa moja basi. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Amina.

224 Wasiwasi, yabisi kavu, na udhaifu, mkakamao, na ugonjwa wa moyo. Unaamini kwa moyo wako wote utapona sasa? Unaweza tu kuendelea moja kwa moja barabarani, ukishangilia tu, ukisema, “Mungu na ashukuriwe,” naye Mungu atakupa ushindi. Unaamini kwa moyo wako wote?

Vema. Mtu mwingine anayekuja sasa? Vema.

225 Utaamini? Vipi kama niliweka tu mikono yangu juu yako, wala sikusema lolote? Unajua ninajua shida yako. Vipi kama ningeweka tu mikono yangu juu yako, ungefikiri...? Wakati ulipopaza sauti pale nje dakika chache zilizopita, vipi kama nilikwambia umekuacha? Ungeamini? Vema. Endelea moja kwa moja. Mshukuru Bwana na uende nyumbani, amini kwa moyo wako wote.

Vema, ninaenda... Vema, mlete mama huyu.

226 Unawazia nini, Dada, unapokuja? Unaamini ya kwamba Yeye...Kama nilisema jambo lolote, ama sikusema lolote, ungepona hata hivyo? Ungeamini hilo kwa vyovyote vile kama ningeweka tu...? Kuna namna fulani ya Roho hapa, mnajua hilo. Unaamini ni Roho wa Bwana aliye juu yetu? Unaamini? Basi mgongo wako unaokusu... Vema, tayari nimekwambia kwa vyovyote vile, kwa hiyo endelea, unaona, endelea, amini, amini, amini kwa moyo wako wote.

227 Ni wangapi wanaoamini, huko nje, kwa mioyo yenu yote sasa? Mnaamini? Yeye ni Mungu. Mnaamini hilo? Yeye ni Mungu juu ya paa la nyumba, Yeye ni Mungu juu ya kanisa, Yeye ni Mungu kanisani, Yeye ni Mungu kila mahali, Yeye ni Mungu.

228 Nilifikiri Nuru hiyo ilikuwa ikimfuata mama fulani, bali ilikuwa ni yule mama mweusi anayeketi pale. Wewe. Naam. Unyamini kwamba mimi ni nabii Wake, ama, mtumishi Wake? Yule mama mweusi aliyeketi pale amevaa kofia nyeupe na nguo nyeupe, unaamini Mungu anaweza kuniambia, wakati unapowasiliana na Roho Wake, una shida gani? Ungekubali jambo hilo? Basi ugonjwa wako wa kibofu hautakusumbua tena.

229 Je, utanipa—utanipa fadhili sasa? Weka mikono yako juu ya mama huyo aliyeketi karibu nawe, maana anasumbuliwa na macho yake. Hiyo ni kweli. Weka mikono yako juu yake. Vema.

230 Utanipa fadhili, unayefuata? Mama aliyeketi karibu nawe anasumbuliwa na kuharisha, kuhara damu, kuharisha. Hiyo ni kweli. Inua mkono wako, weka mkono wako juu yake, omba kwamba huo, atapona.

231 Vipi kuhusu yule mama aliyeketi karibu naye? Unaamini kwa moyo wako wote, Mama? Shida yako iko ubavuni mwako, upande wako wa kulia. Amini kwa moyo wako wote, itakuacha. Unaamini?

232 Vipi kuhusu yule mama aliyeketi karibu naye? Unaamini kwa moyo wako wote? Una vipindi vya kusongwa, huwezi kupata pumzi yako vizuri. Utaipata sasa, maana umekuacha. Amina.

233 Unaamini kwa moyo wako wote? Wekeaneni mikono sasa. Sasa, kwa ajili ya wale walioketi karibu nawe, je, wewe ni mwaminio? Inua mkono wako kama wewe ni mwaminio. Sasa, weka mkono huo unaoamini juu ya mtu mwingine. Haya hapa aliyosema Mungu, Yeye alisema hivi: “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

234 Roho Mtakatifu yuko huko nje, kama tu alivyo hapa juu katika watu hawa; Yuko kila mahali. Mnaamini hilo? Basi mwombe mtu huyo uliyemwekea mkono. Weka mkono wako juu yao na kuomba sasa, mwombe mtu huyo.

235 Baba wa Mbinguni, tunakuletea kusanyiko hili la waaminio, tukikushukuru ya kwamba Uwepo Wako upo hapa pamoja nasi. Hatukuhisi Wewe tu, bali tunakuona ukitenda kazi miongoni mwa watu Wako, ukithibitisha Neno Lako, huku ishara zikifuata.

236 Sasa, kuna wengi wagonjwa katika kusanyiko, saa zimechelewa, lakini Bwana, Wewe ni Mungu mkuu, mwenye nguvu zote, ninaomba ya kwamba utayasikia maombi ya mtumishi Wako, na wakati watu hawa waaminio wamewekeana mikono, wakiomba maombi ya imani, Nawe ulisema, “Kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule, Mungu atamwinua.”

237 Baba, ingetufanya kuwa kundi la wasioamini jinsi gani, kama tusipouamini Uwepo Wako hapa pamoja nasi sasa, baada ya sisi kukuhisi Wewe, kuona Neno Lako, kulihubiri Neno Lako, kuona Neno Lako likitenda kazi kupitia kwetu sote humu jengoni, tukiuhisi Uwepo Wako, tukijua Wewe upo hapa! Na sasa tunatii amri Zako kama waaminio kuwekeana mikono, kwamba kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa huyo.

238 Sasa, Bwana, sikia maombi yangu, ninaweka maombi yangu juu ya madhabahu, ninaweka imani yangu huko juu pamoja nao, na, katika Jina la Yesu Kristo, tunaenda kukabiliana na ibilisi katika changamoto yake ya kutokuamini.

239 Toka, Shetani, kutoka kwa watu hawa, waache. Tunakuamuru, kwa Mungu aliye hai, katika Jina la Yesu Kristo, kuwaacha watu hawa na kuwaondokea, wapate kuponywa.

240 Ninyi nyote mnaoamini ya kwamba mwaminio ameweka mikono yake juu yenu, nawe unaamini ya kwamba Uwepo wa Kristo upo hapa sasa, kama huogopi. . . Kama unaogopa na kusema, “Loo, sijui,” basi mashua yako ndogo huenda ikazama. Lakini kama unaweza kumsikia akisema katika ujumbe Wake, “Usiogope; Ni Mimi, Yesu Kristo,” lile tangazo lenyewe la Biblia lililofanywa liljulikane, kuna imani ya kutosha papa hapa sasa, kama tu hukuogopa. Inaonekana kana kwamba kitu fulani

kinataka kukuzuia, kwamba unasema, “Loo, si—si—si—sijui, ni—nimekuwa mikutanoni hapo awali.”

²⁴¹ Mnaona, ninajua yale mnayowazia hasa. Mnaona, si mimi, ni Yeye anayeniambia. Kama utafanya jambo hili, kumbuka, ninalisema kama mhudumu, kama ndugu yako, laiti ungaliacha mawazo hayo yote yapite kando, na ujue ya kwamba mwaminio amekuwekea mikono!

²⁴² Naye Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Na kama Ibrahimu, baba yetu, alimwamini Mungu kwa muda wa miaka ishirini na mitano kwa ajili ya ahadi, ni zaidi sana vipi Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu unapaswa kuamini ahadi ya Mungu? Je, mnaikubali? Mnaamini hilo? Na kama mnaamini ni kweli, mtoleeni Mungu ushuhuda, simameni kwa miguu yenu katika ushuhuda kwamba, “Sasa ninakubali uponyaji wangu. Ninaamini ya kwamba nimeponywa, kwa sababu niko katika Uwepo wa Mungu na mwaminio ameniwekea mikono.” Asifiwe Mungu Yule atupaye ushindi! Amina. 🐦

62-0620 Msiogope
Great Western Exhibit Center
South Gate, California Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org